# UMOJA WETU NA KRISTO

Somo la Kuishi kwa Neema katika Imani

Na David Kuykendall

Kimechapishwa na
**Huduma ya David Kuykendall**
**Dallas, Texas**

**© 2006**
**David Kuykendall**

# Yaliyomo


| | | |
|---|---|---|
| 1. | Je Una Uzima Tele Tele | 1 |
| 2. | Yesu Kristo, Adamu wa Mwisho | 3 |
| 3. | Kuelewa Dhambi | 5 |
| 4. | Kusulubishwa, Kuzikwa, Kufufuliwa Na Kuketishwa | 8 |
| 5. | Tunapokea Neema kwa Njia Gani? | 10 |
| 6. | Amri Nne Katika Warumi 6:12-13 | 12 |
| 7. | Maisha ya Kujazwa na Roho | 14 |
| 8. | Tofauti Inayoletwa na Roho | 16 |
| 9. | Uhuru Kutoka kwa Dhambi | 20 |
| 10. | Uhuru Kutoka kwa Ulimwengu | 23 |
| 11. | Uhuru Kutoka kwa Sheria | 25 |
| 12. | Maisha Katika Maeneo ya Mbinguni | 29 |
| | Ziada | 32 |
| | Neno la Mwisho Kutoka kwa Mwandishi | |




Inatupasa kutii maneno ya Paulo yaliyoandikwa katika 1 Wathesalonike 5:18 ya kwamba tutoe shukurani katika mambo yote. Hii haimaanishi kushukuru bila kujali hali zilizopo. Inamaanisha kushukuru kwa ajili ya mambo yote. Wengi wamepata hali zao zimebadilika baada ya kufanya hivyo; na wengi na wamepata amani katikati ya hali zao ngumu kwa kutoa shukurani.

*Jaribu!*

**NENO LA MWISHO KUTOKA KWA MWANDISHI**

Kuweza kukuletea kweli hizi za Mungu zinazo badili-maisha, ni fursa kubwa sana kwetu. Kwa miaka mingi, tumekuwa na hii fursa ya kushiriki kweli hizi, na matokeo yamekuwa ni kuwaona wengi wakiingia katika maisha ya uzima tele tele. Ni ombi letu kwamba utapokea na kufanyisha mazoezi yale yote ambayo umefundishwa katika kurasa hizi.

Tumegundua kwamba wale wote ambao wanapokea na kutumia kweli hizi, huingia katika huduma mpya kabisa. Kuna uwezekano kwamba kwa miaka mingi umekuwa na huduma ya kupeleka injili kwa wale ambao bado hawajaokoka. Wale ambao wanaanza kuishi katika umoja wao na Kristo, wanagundua kwamba wako na huduma nyingine ya kubadili-maisha. Hii ni kufundisha waamini wengine kuhusu kusulubishwa, kuzikwa, na kufufuliwa rohoni. Itakuwa furaha kubwa kusikia waamini wengine wakieleza yale ambayo Mungu ametenda katika maisha yao.

mbinguni tangu walipompokea Yesu kama mwokozi wao. Ila, wataweza kuyajua maisha haya wakati watakapoamini kwamba wameketishwa katika maeneo ya mbinguni, na kuchagua kuishi maisha katika makubaliano haya.

Kwa huzuni, waamini wengi hawajui nafasi yao katika Kristo na kwa hivyo hawaishi kulingana na ukweli huu. Ni lazima wasulubishwe pamoja na Kristo kabla ya kuketishwa juu ya kiti Chake cha enzi. Hata hivyo, watakapo pitia mambo haya, Baraka za rohoni zitamiminika kutoka kwa chanzo kisichopungua. Kisha maisha yao yatakuwa yenye uchangamfu kila siku!

**ZIADA**
**NAFASI YA MATESO KATIKA MAISHA YA NEEMA**

Kuna mawazo tofauti kuhusu kuteseka kwa Wakristo. Wengine hufundisha kwamba Wakristo hawastahili kuteseka. Wengine hufikiri kwamba mateso ni ishara kwamba mtu ametenda dhambi na Mungu anamwadhibu.

Mwiba-katika-mwili wa Mtume Paulo, unatupatia ufahamu mpya kabisa kuhusu mateso. Mwiba-katika-mwili wa Paulo, ulimuweka katika hali ya unyonge. Maelezo ya Paulo kuhusu mateso yake yanadhihirisha kwamba alihofia kuwa yangekuwa kizuizi kwa huduma yake. Paulo alimuomba Bwana mara tatu ili auondoe. Jibu la Bwana kwa maombi yake ilikua, “Neema yangu inakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu” (2 Wakorintho12:9a). Paulo kisha akaongeza, “Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu” (2 Wakorintho 12:9b). Mateso ya Paulo yaliondoa hali ya kujiamini mwenyewe na kumlazimisha kumtumaini Mungu ili apate kuishi na kutumika kwa neema ya Mungu.

Kuna mambo mengine muhimu yaliyotajwa katika Maandiko ambayo yanasababisha tuteseke tunapoishi katika umoja wetu na Kristo. 2 Timotheo 3:12 anasema, “Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa.” Yesu anasema katika Yohana 15:19, “Kama mngekuwa wa ulimmwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali mimi niliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia.”

Hata mateso yaliyotajwa katika kifungu kilichotangulia yanamsababisha muumini katika imani kumwangukia Mungu-na matokeo yake ni kupokea neema ya Mungu. Mateso yanatuweka chini ya neema. Kuishi kulingana na yale mambo tano muhimu inatuweka chini ya neema.

Kuna matokeo mengine yanayotokana na mateso na ambayo yanatokana na mtu kuishi maisha ya kufa, kuzikwa, na kufufuka. Kitabu cha Waebrania kiliandikiwa Wakristo waliokuwa wanateseka. Katika mlango wa kumi na mbili, hawa watoto wa Mungu waliambiwa, “Maana ni hakika, hao kwa siku chache waliturudi kama walivyoona vema wenyewe; bali yeye kwa faida yetu, ili tuushiriki utakatifu wake. Kila adhabu wakati wake haionekani kuwa kitu cha furaha, bali cha huzuni; lakini baadaye huwaletea wao waliozoezwa nayo matunda ya haki yenye amani” (Waebrania 12:10-11). Utakatifu na uhaki ni matokeo ya mtu anayeishi maisha ya kusulubishwa, kuzikwa, na kufufuka.

Ikiwa umekumbana na idadi isiyo ya kawaida ya changa moto ngumu kuanzia ulipoanza kuishi kwa neema kulingana na Warumi 6, basi jua kwamba Mungu amezileta kwako ili zikuwezeshe kukua katika maisha mapya.



## SURA YA KWANZA: JE, UNA UZIMA TELE TELE?

Je, umeshawahi, mara kwa mara, kujitambua kama Mkristo aliyeshindwa? Je, unafanya na kuwaza mambo yanayokusababisha ujichukie mwenyewe? Je, unahisi katika roho ya kwamba huwezi kufanya mambo mengi ambayo unatamani kufanya – na unajua kua unastahili kuyafanya?
Ikiwa jibu lako kwa haya maswali ni ndio, basi wewe ndiye ambaye umeandikiwa kitabu hiki. Sote twaweza kutoa shuhuda za kushindwa kwetu. Tunahitaji kitu - ukweli utakao badilisha maisha yetu. Hapa kuna baadhi ya shuhuda kutoka kwa watu ambao wanajihisi kama walioshindwa na wanataka suluhisho.

- “Nimejawa na hofu. Kila wakati ninaogopa ya kuwa jambo mbaya litampata mmoja wa jamii yangu. Ninajua kuwa inanipasa kushuhudia, lakini ninaogopa kukataliwa. Marafiki wangu wananijua kama mwenye wasiwasi. Ninashikwa na wasiwasi kuhusu kila kitu. Kwa miaka mingi nimeomba kuhusu hofu zangu, lakini ninazidi kuwa na hofu kama niliyokua nayo kabla sijawa Mkristo.”
- “Nawapenda watoto wangu, lakini kila siku ninatenda dhambi ya kuwakasirikia. ninashindwa kuwavumilia kwa upesi. Nimeomba kuhusu swala hilo lakini sipati ushindi.”
- “Nina tatizo la kushikwa na tamaa ya mwili kila wakati. Ninajisikia kama Mkristo mwovu, ghadhabu niliyonayo mara nyingine huzidi. Nimejaribu kila kitu nijuacho nipate ushindi, lakini sijui nitageuka namna gani.”

“Uchungu ndiyo shida yangu. Marafiki wangu Wakristo hutumia udhaifu wangu, na sijioni nikipata ushindi. Kila siku ninawafikiria na yale waliyonifanya. Wakati niko pamoja nao, siwafanyii kama invyonipasa. nitawezaje kuwasamee? “Maombi hayajanisaidia hata kidogo.”
“Sina imani hata kidogo. Ninawaona wengine ambao wanaweza kuchukua hatua ya imani na miujiza inatendeka. Mbona sina imani kama yao?”

- “Ijapokua ninampenda Bwana kwa dhati, sijapata ufanisi katika kuwaongoza wengine kumpokea Kristo. Ninajaribu niwezavyo, ila juhudi zangu zinaambulia patupu.”
- Baada ya kumpokea Kristo, nilijawa na furaha na imani. Sijapata kujiskia namna hiyo kwa muda mrefu. Hivi sasa, huzuni nzito ndiyo imejaa maishani zaidi ya furaha na imani.”

Kuna uwezekano kwamba unajitambua kuwa na shida moja au zaidi kati ya zile zilizonakiliwa hapa. Huenda unasema, “Zaidi ya kuwa na zile shida zilizo tajwa hapa, pia nina zingine ambazo ninaamini kuwa ni mbaya zaidi ya zile zilizotajwa. Je ninaweza kupata msaada?” Ndio, unaweza kupata msaada! Tunapokea nguvu tunazozitafuta kwa kuelewa na kuishi katika umoja wetu na Kristo, katika mauti yake, kuzikwa na kufufuka. Unahitaji kuelewa na kukubaliana na zile kweli zinazozungumziwa katika kurasa zifuatazo ikiwa unataka maisha yako yabadilike. Matokeo yake yatasababisha uhusiano wako na Bwana kuwa wa karibu na hii ndiyo jambo la muhimu zaidi katika maisha yako.

Katika Wakorintho 6:17, mtume Paulo anafafanua, “ *………mmeunganishwa pamoja……* ” Hata hivyo, Wakristo wengi hawaelewi kwamba wakati tulipompokea Kristo, tuliunganishwa pamoja na Bwana ambae alisulubishwa, akazikwa na akafufuka. Kwa hivyo, ili kwamba utimilifu wa maisha na ufanisi wa hali ya juu katika utumishi wa Kikristo, waaminio ni lazima waelewe na kupitia maisha ambayo msingi wake ni umoja na Kristo.

Waamini wengi wanaelewa kwamba Kristo anaishi ndani ya kila muumini. Ijapokuwa hii inatusaidia katika kuelewa na kupitia, kipekee haitatupatia maisha ya kiroho na yenye matunda kama tunavyotaka. Hivyo basi, ni lazima pia tuelewe na tutumie ukweli mwingine muhimu, unaofundishwa katika Agano Jipya kuhusu umoja wetu na Kristo. Ukweli huu unafafanuliwa kwa njia nyingi katika Maandiko kama: kuwa "ndani Yake", "katika Kristo Yesu", "ambaye ndani Yake", au "ndani ya mpendwa". Mataamshi haya yote yanamaanisha kitu kimoja — kwamba kila Mkristo yuko katika umoja na Kristo. Ni muhimu sana kuelewa kwamba yule Kristo akaaye ndani yetu hatendelea kutujaza na uwepo wake, au kufunuliwa kupitia kwa maisha yetu, mpaka tutakapoutumia ukweli kwamba, sio tu kuwa Yesu yuko ndani yetu, lakini pia sisi tuko ndani Yake. Wakati Mkristo, kwa ukweli anaelewa na kutumia ufunuo huu, kutakuwa na mabadiliko makubwa katika maisha na huduma yake.

Katika hichi kitabu, maneno "umoja wetu na Kristo" na "muungano wetu na Kristo" yanatumika kumaanisha kitu kimoja. Pia, "maisha ya neema" au "maisha ya imani" yanatumika kufafanua ujuzi wa wale ambao wanaishi katika muungano wao na Kristo.

Ikiwa maisha yako sasa yanaendelea vizuri, kuna uwezekano kitabu hiki utakiona kuwa cha kufurahisha, lakini bila kuwa na umuhimu mkubwa maishani mwako. Hata hivyo, huenda ukawa mtu aliyevunjika moyo na kutahayarishwa na maisha yake ya wokovu na hatimaye umefikia mwisho wako na ubatili wa juhudi zako za kubadilika. Ikiwa hiyo ni kweli, huenda ukawa katika mwanzo wa kuishi maisha ambayo umeyatamani na kuyatafuta tangu ulipookolewa. Katika Yohana 10:10, Yesu anayaita "uzima tele".



kwamba kitabu chote ni nakala ya matendo ya Yesu Kristo. Basi tunaweza kuelewa kwamba matendo yote ya waaminio yaliyofafanuliwa katika kitabu chote cha Matendo yalikuwa kwa uhakika, ni kazi za Yesu Kristo. Tunapochambua kitabu hichi, tunaona kwamba Yesu alitenda kazi zake kupitia kwa waamini waliokuwa wakitencda mapenzi yake hapa duniani.

Kila wakati, Yesu anafanya kazi yake na kujenga Kanisa lake kupitia kwa waamini. Ni lazima atuongoze kwa kutuonyesha mpango wake duniani siku ya leo. Hivyo basi, ni lazima tujifunze yale anayotamani kutenda ndani yetu na kupitia ndani yetu ili tusifanye kulingana na mipango yetu wenyewe na hekima yetu.

Bwana wetu alisema kwamba yote aliyoyafanya ilikuwa ni kwa sababu Baba Yake alikuwa akiifanya ndani yake. *"Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nane ninatenda kazi. Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile. "* (Yohana 5:17,19) *"Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake."* (Yohana 14:10)

Maombezi ni sehemu mojawapo ya huduma yetu kwa wengine. Wakati tunaomba kutoka kwa nafasi yetu kwenye kiti cha enzi na Bwana Yesu Kristo katika maeneo ya mbinguni, tunaongeza umakini wetu kama waombezi. Katika 1Yohana 5:14-15, tunajifunza kwamba maombi yatajibiwa kulingana na mapenzi ya Mungu. Kwa hivyo, nafasi yetu katika kuwaletea wengine Baraka kupitia kwa maombi, ni kwa kuyajua mapenzi Yake na kuomba kwamba atimize tamanio Zake katika maisha yao. Jinsi ya kujua tamanio za Mungu kwa watu wengine ni kupitia kwa ushirika wa karibu pamoja naye katika maeneo ya mbinguni. Paulo katika Wafilipi 3:10, anaeleza kuwa hakutaka tu kumjua Yesu Kristo na uweza wa kufufuka Kwake, ila pia alitaka kujua *"ushirika wa mateso Yake."* Katika Warumi 9:2, Paulo anazungumza kuhusu uzito mkubwa na majonzi yasiyoisha moyoni mwake kwa ajili ya Wayahudi wasioamini. Ni hakika kwamba, majonzi ambayo Paulo alihisi yalitoka moyoni mwa Mungu. Wakati mateso ya Yesu au maumivu Yake yanamiminika katika mioyo yetu, hivyo ndivyo kujua "ushirika wa mateso Yake." Paulo aliweza kuwa na huu mzigo kwa sababu aliweza kuwa na ushirika wa karibu na Kristo kwa kuishi maisha katika maeneo ya mbinguni. Shetani ni adui yetu mkatili sana. Kusudi lake ni kutuondoa kutoka kwa mpango wa Mungu wa maisha yetu. Katika Waefeso 1 :18-23, Paulo anawasilisha tamanio lake kwamba wanaoamini watajua nafasi yao ya mamlaka juu ya shetani katika maeneo ya mbinguni. Anaomba *"Macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo; na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake;aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote."*

Tunaweza kuona kutoka kwa ombi hili ya kwamba, Paulo anajua kuwa Shetani ni adui aliyeshindwa kabisa na ambaye yuko chini ya miguu yake kwa sababu ya kazi ya Kristo. Kwa hivyo anaweza kumkabili kutoka kwa nafasi ya mamlaka. Tunaweza kuwa na huu ujasiri juu ya Shetani ikiwa tutachagua kuishi maisha katika maeneo ya mbinguni.

Waamini wote wameketishwa pamoja na Kristo juu ya kiti Chake cha enzi katika maeneo ya

kuchukua hiyo nafasi. Kifungu kingine kinapatikana katika Wafilipi 3:1-8. Paulo anaelezea kuhusu tamanio yake kubwa ya kumjua Kristo na kwamba anatambua kitu chochote kinachomzuilia katika juhudi za kumjua Kristo kuwa takataka ama upuzi.

Mahali pa tatu ambapo tunayaona mambo haya, ni katika ombi la Bwana wetu kwa Baba Yake kabla ya kusulubishwa. Aliomba akasema, *"na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma"* (Yohana 17:3). Neno lililotafsiriwa "kujua" ni lile neno linalotumika kwa ujuzi wa kupitia. Kumjua Mungu Baba na Mungu Mwana kwa ujuzi ni kuwa na uzima wa milele. Kifungu cha nne kinapatikana katika Waebrania 12:2. Hapo tunajifunza kwamba, uweza wa kukabiliana na hali ngumu maishani, unapatikana kwa *"Kumtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu."* Hii inatuhimiza kwamba tuelekeze mtazamo wetu kwa Yesu Kristo. Njia pekee ambayo tunaweza kuwa na ushirika wa kuendelea na Bwana, ni katika ujuzi wa umoja wetu na Kristo kwa kuishi katika maeneo ya mbinguni. Tukiwa katika hii nafasi, kuabudu kwetu kunasonga katika kiwango cha juu zaidi.

Agano Mpya haituambii ni ipi iliyo ya muhimu zaidi – kuabudu au kutumika. Inatufundisha kwamba tunaweza kutenda yote mawili kwa wakati mmoja. Paulo anasema katika Waefeso 2:5-7, *"Hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema. Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu; ili katika zamani zinazokuja audhirishe wingi wa neema yake upitayo kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu."* Katika kifungu cha 8, tunaona kwamba tunapokea neema kupitia kwa imani. *" Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu."* Bwana wetu anakusudia kwamba, maisha ya muumini yatakuwa maisha ya kuendelea katika imani. Tunapoishi kwa imani, Maandiko yanatuambia kwamba "mito ya maji ya uzima" itatiririka kutoka kwetu na tutatenda hata miujiza mikubwa kuliko ambayo Yesu alifanya. (Yohana 7:38 na Yohana 14:12)

Katika Wakolosai 3:4, Paulo anandika, *"Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu."* Hichi si kifungu kinachozungumza kuhusu siku za usoni. Paulo anataka tuelewe kwamba ufunuo huu wa Yesu Kristo ni kitu ambacho tunaweza kukipitia katika wakati wa sasa. Kinapitiwa na wale ambao wanaishi katika "maeneo ya mbinguni."
Katika Wafilipi 3:10, Paulo alisema kwamba tamanio yake kubwa maishani ilikuwa kumjua Yesu Kristo. Pia anasema anataka kutambua "uweza wa kufufuka kwake". Hiyo ndio iliyokuwa tamanio yake ya kumjua Kristo kwa kuketishwa pamoja Naye katika kiti chake cha enzi katika maeneo ya mbinguni.

Bwana wetu alimwarifu Simoni Petero kwamba alikuwa mtu aliyebarikiwa na Mungu kwa sababu alipokea ufunuo kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo (Mathayo 16:15-17). Hata sisi pia tunaweza kubarikiwa kama yeye kwa kuishi maisha ambapo tunatambua kukeketishwa pamoja Naye kwa kiti chake cha enzi na kupata Kristo akifunuliwa maishani mwetu. Hebu waza baraka za kuishi maisha ambapo tunaendelea kupokea ufunuo wa Bwana wetu Yesu Kristo!
Katika Wakolosai 3:4, Paulo anamtambulisha Kristo kama "*uzima wetu*". Hii inatukumbusha madai ya Bwana wetu katika Yohana 14:6, *"…Mimi ndimi njia, na kweli, na UZIMA."* Na Paulo anatoa ushuhuda wake katika Wagalatia 2:20, *"Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu."* Kifungu cha kwanza cha Matendo, kinatufunulia



**SURA YA PILI: YESU KRISTO, ADAMU WA MWISHO**

Tunaamini kuwa Yesu anatupenda kwa sababu Biblia inatuambia kwamba Anatupenda — hata kama tunajisikia kuwa tunapendeka au la. Biblia ndiyo mamlaka yetu kuhusu maswala ya kiroho, na kama matokeo, tunakubali mafundisho yake bila kujali hisia zetu au mawazo.
Kwa hivyo, ni muhimu kuelewa kweli za Biblia za msingi kuhusu umoja wetu na Kristo. Kuna uwezekano kwamba kweli hizi ni mpya kwako. Lakini ni lazima zieleweke ikiwa tutapata ubora wa maisha ambayo Bwana amewezesha. Kwa imani, fungua moyo wako kwa Bwana na umwambie kwamba unaamini kuwa Atakuelezea kuhusu ukweli Wake.

Mojawapo wa njia ambazo ukuu wa Bwana umefunuliwa ni kupitia majina ambayo yanamfafanua katika Maandiko. Anaitwa, "Njia, Ukweli na Uzima", "Mkate wa Uzima", "Nuru ya Ulimwengu" na "Mwana Kondo wa Mungu". Lakini mmojawapo wa cheo muhimu zaidi ni ufafanuzi wa Paulo kuwa ni "Adamu wa Mwisho". Warumi 5:14 inamfafanua Adamu kama "picha ya Kristo". Picha ni mfano. Hivyo basi, tunaona kwamba Adamu ni kama Yesu. Kwa uhakika, Adamu amefanana Naye, mpaka Yesu anaitwa, "Adamu wa Mwisho".

Ni rahisi kuelewa tofauti kuu zilizoko kati ya Adamu na Yesu. Adamu alileta dhambi na mauti duniani; Yesu akaleta haki na uzima. Lakini tunashangaa, ni katika njia gani ambapo Adamu na Yesu wanafanana? Jibu ni: kila mmoja ni kichwa cha uzao. Adamu ndiye kichwa cha uzao wa kiasili na Yesu ni kichwa cha uzao wa kiroho.

Kama kichwa cha uzao wa kiasili (uzao wa binadamu), Adamu aliathiri wote waliozaliwa katika uzao huo. Habari hii kwamba mtu mmoja, Adamu, aliathiri wote waliozaliwa katika uzao wa binadamu, ni picha ya Yesu na uguso wake kwa wote "waliozaliwa tena" katika uzao wake wa kiroho. 1 Wakorintho 15:49 inamwita Yesu "Adamu wa Mwisho" na pia inasema, *"Kama vile tulivyoichukua sura yake yule wa udongo, kadhalika tutaichukua sura yake yeye aliye wa mbinguni."* Kifungu hichi kinahusu ufufuo na kinafundisha kwamba tutapokea miili kama ule wa Bwana Yesu alipofufuka wakati atakaporudi.
Kitu cha kwanza ambacho tunashirikiana na Adamu, akiwa kichwa cha uzao wa binadamu, ni mwili wake wa asili. Wote waliozaliwa kwa njia ya kawaida wako na mwili wa binadamu ambao Mungu alimpa Adamu alipomuumba. Kitu cha pili kilichotokana na Adamu kuwa kichwa juu ya uzao wote wa binadamu ni hali yake ya dhambi. Katika Warumi 5:12, Paulo anaandika, *"Kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni"*. Na katika msitari wa 19, Paulo anatangaza, *"Kwa kuasi kwake mtu mmoja, watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi"*.

Wakati Adamu alimuasi Mungu na akala kutoka kwa mti usiofaa, kando na kujiletea shida ya dhambi yeye mwenyewe, pia aliipitisha kwa kila mtu aliyezaliwa katika uzao wake — isipokuwa kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mwanadamu aliye mkamilifu. Warumi 5: 12-13 inatuambia kwamba Adamu kando na kusababisha tuwe na shida ya dhambi pia alisababisha tuwe na shida ya mauti. Sote tunaishi katika mauti kwa sababu ya kile Adamu alichokifanya. Mungu alimuondoa pamoja na Hawa kutoka kwa Bustani ya Edeni ili wasile kutoka kwa mti wa uzima na wakaishi milele hapa duniani katika hali yao ya dhambi. Pia hukumu ya mauti ya kimwili ya siku za usoni ilitolewa juu yao na pia kwa kizazi chote cha wanadamu kwa sababu sisi ni uzao wake. Wakati tunapozaliwa katika uzao wa Adamu, tunazaliwa na mbegu za mauti katika miili yetu. 1 Wakorintho 15:22 inatuambia, *"Katika Adamu, wote wanakufa."*

Kutoka kwa somo hili la Adamu na uzao wake, tumedhiditisha ukweli ufuatao: Tulipozaliwa katika uzao wa Adamu, yale mambo yaliyokuwa kweli kuhusu Adamu, yalikuwa pia kweli kutuhusu. Yesu anaitwa “Adamu wa Mwisho”. Hii inafunua ukweli mwingine muhimu zaidi kwamba, wakati “tulizaliwa tena” na tukaingia katika uzao wa Yesu, mambo yaliyo kweli kumhusu Yesu, yakawa kweli pia kutuhusu. Kwa hivyo tunapoelewa wazo la Yesu kama “Adamu wa Mwisho”, basi tutaelewa yale ambayo yamekuwa kweli kutuhusu kama wanachama wa uzao wake.

Kweli hizi zimeonyeshwa kwa uwazi katika Warumi 6:3-5 ambayo inasema: *“Hamfahamu yakuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo nasi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake.”*

Tulipoingia katika uzao wa Yesu, tulisulubishwa, tukazikwa na tukafufuka. Milango ifuatayo itaelezea pamoja, maana ya kusulubishwa, kuzikwa na kufufuka kwetu na pia itatuonyesha jinsi Yesu alivyoandaa urithi wenye utele kwa waamini wote wanaopitia hali hizo.



## SURA YA KUMI NA MBILI: MAISHA KATIKA MAENEO YA MBINGUNI

Uwezekano wa maisha katika maeneo ya mbinguni ni somo ambalo linafunzwa kwa wingi katika Maandiko. Katika Waefeso 2:5-6, Paulo anatuonyesha kwamba kufufuka kwetu na Kristo kunamaanisha mambo matatu: 1) tumefanywa kuwa hai; 2) tumefufuliwa kutoka kwa wafu, na 3) tumeketishwa katika maeneo ya mbinguni. Katika kila tamko, anatumia maneno ya wakati uliopita. Hii inamaanisha kwamba imeshatendeka.

Katika Wakolosai 3:1-4, Paulo anaandika, *“Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameeketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu.”*

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania pia anatangaza hili wazo la kuishi katika maeneo ya mbinguni. Mwongozo wake ni tofauti kidogo kuliko vifungu vilivyo tajwa hapo awali, lakini lile wazo bado liko wazi. Anandika: *“Basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu, njia ile aliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pazia, yaani, mwili wake; na kuwa kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu; na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi.”* (Waebrania 10:19-22)

Yesu akasema, *“Wala hakuna mtu aliyepaa mbinguni, ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni, yaani, Mwana wa Adamu.”* (Yohana 3:13). Mara nyingi Alishudia kwamba mambo yale aliyoyaona na kusikia ndiyo aliyotenda peke yake. Yesu alipitia hali ya kuishi katika maeneo ya mbinguni katika maisha yake hapa duniani. Halafu, kabla tu ya kupaa Kwake, Akawaambia, *“…Amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma mimi,mimi nami nawapeleka ninyi.”* (Yohana 20:21). Kati ya mambo mengine mengi, hii inamaanisha kwamba tunastahili kupitia hali za maisha kama zile alizozipitia.

Kuishi katika maeneo ya mbinguni wakati bado tunaishi hapa duniani, inamaanisha kwamba waumini wanaishi katika dunia mbili wakati mmoja. Waebrania 10:24 inatuambia, *“Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri.”* Tunaitii hiyo amri kwa kuishi katika dunia mbili wakati mmoja. Matamshi ya Bwana wetu kuhusu maisha yake mwenyewe, inamaanisha kwa uwazi kwamba aliishi katika dunia zote mbili kwa wakati mmoja alipokuwa hapa duniani.
Baraka za maisha haya ziko tele. Kuna Baraka kwa ajili yetu na pia sisi tunawabariki wengine. Kuabudu na uhusiano wa kibinafsi na Mungu huonenekana kama si mambo ya umuhimu sana kwa watu wengi ikilinganishwa na utumishi wao. Hii hujitokeza mara nyingi katika viongozi wa kiroho ambao wanakuwa na bidii katika huduma zao za Kikristo. Lakini vifungu vingi vya Maandiko, vinatuonyesha kwamba kuabudu kwetu ndio jambo la muhimu zaidi.

Kifungu cha kwanza ambacho tutatazama kinapatikana katika Luka 10:41-42. Bwana anamkemea Martha kwa sababu ya nia yake kumhusu Mariamu, ambaye tamanio yake ilikuwa kuketi na kumsikiliza Yesu badala ya kumsaidia Martha kuandaa chakula. Anamwambia Martha, *“Kitu kimoja kikahitajika”*. Basi tunaona kwamba, kuwa katika uwepo wa Bwana wetu ndiyo jambo la umuhimu zaidi. Je, hii inamaanisha kwamba tuwe wavivu? La, haimaanishi hivyo! Lakini inamaanisha kwamba huduma itafuata na itakuwa matokeo yetu ya kumwabudu Bwana, wala sio

kwanza katika maisha yao.

Sababu moja Roho Mtakatifu atatuweka katika Neno ni kwamba, jinsi tunavyokuwa na ufahamu mwingi wa Biblia, ndivyo tutakavyoweza kutambua kwa wingi, ikiwa tamanio tuliyo nayo katika kutenda jambo ni amri kutoka kwa Roho Mtakatifu au inatokana na mwili wetu. Wakati Roho Mtakatifu anatuongoza katika kutenda kitu kilichoamriwa katika Maandiko, hua pia Anatupatia nguvu za kuweza kutenda jambo lile. Tunapojaribu kudumisha amri kwa nguvu zetu wenyewe, tunakosa uweza na hatutafanikiwa.



## SURA YA TATU: KUELEWA DHAMBI

Ikiwa tutapata uzima tele, ni lazima pia tupatane na umoja wetu na Kristo katika kusulubishwa, kuzikwa na kufufuka. Mlango huu umeandikwa kwa ajili ya kutuandaa kwa haya.

Kushindwa kwetu kiroho kumekuwa na uchungu na mara kwa mara kugandamiza. Kumetusababisha kujua kwamba tuliingia katika ulimwengu huu tukiwa na hali ya dhambi — na kwamba inaendelea kufanya kazi hata baada ya kuokoka. Mpaka tutakapokubali, kutambua na kuielewa shida yetu ya dhambi, tutaishi maisha yetu yote tukikabiliana na dhambi maalum bila ya kushughulikia chanzo chake.

Agano Jipya inatumia maneno matatu kufafanua shida yetu ya dhambi: "Dhambi", "mtu wa kale" na "mwili". Agano ya Kale inatumia neno la nne, "Ufahamu wa mema na mabaya". Hii inapatikana katika mlango wa pili na wa tatu wa Mwanzo. Tutaona maana ya neno hilo kwa kuangalia baadhi ya vifungu katika Mwanzo vinavyotuonyesha chanzo cha hali yetu ya dhambi.

> Mwanzo 2:9: *Bwana Mungu akachipusha katika ardhi kila mti unaotamanika kwa macho na kufaa kwa kuliwa; na mti wa uzima katikati ya bustani, na mti wa ujuzi wa mema na mabaya* .
> Mwanzo 2:16-17: *Bwana Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, "Matunda ya kila mt iwa bustani waweza kula, walakini matunda ya mtu wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mtu huo utakufa hakika."*
> Mwanzo 3:1-3: *Akamwambia [nyoka] mwanamke, "Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?" Mwanamke akamwambia nyoka, "Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio wa katikati ya bustani Mungu amesema, 'Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa.'"*
> Mwanzo 3:4-6: *Nyoka akamwambia mwanamke, "Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya". Mwanamke alipoona ya kuwa mti ule wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala.*
> Mwanzo 3:11, 12: *Akasema [Bwana Mungu], "Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale? Adamu akasema, Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, name nikala."*
> Mwanzo 3:22, 23: *Bwana Mungu akasema, "Basi huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya; na sasa asije akanyosha mkono wake akatwaa matunda ya mti wa uzima, akala, akaishi milele;" kwa hiyo Bwana Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa."*

Vifungu hivi vinatuonyesha kwamba Adamu aliiharibu nafsi yake kwa ujuzi wa mema na mabaya. Na halafu akatupitishia huo uharibifu. Tunahitaji kuelewa inamaanisha nini kusema kwamba Adamu aliiharibu nafsi yake kwa ujuzi wa mema na mabaya na sasa nafsi zetu pia zimeharibiwa vile vile.

Warumi 1:18-22 inanakili hadithi mbaya kuhusu mwanadamu kumkataa Mungu na uzorotaji wa

tabia na roho ambao ulifuatilia. Sababu moja iliyochangia tukio hili la kukataa Mungu na kuleta uzorotaji uliofuatilia ni kwamba *"walidai kuwa na hekima lakini wakawa wapumbavu"* (kif.22). Sasa ni dhahiri kwamba imani duni na yenye hasara kuwa sisi tunayo hekima kando na Mungu ndiyo "ujuzi wa mema na mabaya". Katika kitabu hiki, tutazungumza kuhusu njia ambazo imani hii ya uharibifu inavyotuadhiri. Tutaona kwamba ikiwa hatutaikabili kikamilifu, itatawala maisha yetu kama mtawala katili wa ki-imla. Tamshi hili, "ujuzi wa mema na mabaya" (nia ya kiburi na kujitosheleza) inazungumza kuhusu hali yetu hatari ya dhambi.

Nia hii tunaiona katika wanadamu kila mahali. Haijui mipaka yoyote. Tunatoa hukumu kuhusu kila kitu na juu ya kila mtu. Tunajaribu kuwafanyia wengine maamuzi – kwa sababu ya udanganyifu wa kufikiri kwamba tunajua zaidi yaliyo bora. Kwa hakika, hata tunafikiria kuwa tunajua zaidi ya Mungu. Matatizo mengi mazito yamejitokeza makanisani na huzuni nyingi na uchungu mwingi kusababishwa kwa sababu muumini mmoja anafikiri kwamba anajua kila kitu na kwamba mtizamo wake ndio bora zaidi.

Hili tatizo la dhambi huanzia katika mawazo yetu na kujitokeza katika matendo yetu. Mithali 23:7 inasema, *"Kama [mwanadamu] awazavyo moyoni mwake, ndivyo alivyo."* Hii ndiyo sababu Paulo anatuambia katika Warumi 12:2 kwa lazima tugeuzwe kwa "kufanywa upya katika nia zetu". Neno hili "kutubu" linatokana na maneno mawili ya Kiyunani "kubadilisha nia". Ni lazima tuelewe matamshi matatu ya Agano Jipya ambayo yanafafanua tatizo letu la dhambi ambalo tumeshalitaja. Maneno haya ni: "dhambi", "mtu wa kale" na "mwili". Tutayachambua na kujaribu kuyaelewa vizuri zaidi. "dhambi", inapotumika katika Agano Jipya kuzungumza kuhusu hali yetu ya dhambi, inapasa kueleweka kama "ujuzi wa mema na mabaya". Hili tamshi "mtu wa kale", linazungumza kuhusu mtu ambaye tulifanyika kwa kuzaliwa katika kizazi cha Adamu. Mtu wetu wa kale ni matokeo ya nia ya kufikiri kuwa tunajua kila kitu na kwamba tunajitosheleza. Tamko, "mwili", pia linatumika kuzungumza kuhusu tatizo letu la dhambi. Ijapokuwa mwili na mtu wa kale hazimaanishi kitu kimoja, mwili ndiyo kiini cha mtu wa kale.

Hivi basi, mwili wetu ni nini? Mwili wetu ni nia ya kufikiri kwamba tunajua kila kitu. Tunapoishi katika mwili, (na wala sio katika roho) tunakuwa na ujasiri katika sisi wenyewe, katika uweza wetu, katika hekima yetu. Kwa hivyo katika hiyo hali, mwili na ujuzi wa mema na mabaya inakuwa na maana sawa. Hii imeonyeshwa katika Agano la Kale wakati Musa alikuwa akiwapa Wanaisraeli Amri, agano lililotakatifu kati ya wana wa Israeli na Mungu. Katika nyakati tatu tofauti, watu walimwambia Musa, *"Tutafanya yale yote ambayo Bwana amesema"* (Kutoka 19:8, 24:3, 7). Bila shaka huu ulikuwa ni ujasiri wa nafsi zao ukizungumza kwa sauti na kwa uwazi ulikuwa ni udhihirisho wa mwili wao. Kwa sababu, kadri muda ulivyosonga, ilidhihirika ya kwamba sio tu kuwa hawengeweza kuitii Amri kikamilifu, ila walikuwa wakaidi kiasi cha upotofu katika sehemu kubwa ya historia yao. Kwa uhakika, hata kabla ya kifo cha Musa na miaka arobaini kupita tangu walipopatiwa Amri juu ya Mlima Sinai, Musa aliwapa hili neno kutoka kwa Bwana lililotabiri kuwa watashindwa kutenda yale waliyokuwa wamemwahidi Bwana kwa ujasiri kwamba wangetenda. *"Kwa kuwa nitakapokwisha kuwatia katika nchi niliyowaapia baba zao, imiminikayo maziwa na asali; nao watakapokwisha kula na kushiba, na kuwanda; ndipo watakapoigeukia hiyo miungu mingine, na kuitumikia, na kunidharau mimi, na kulivunja agano langu.* (Kumbumubu la Torati 31:20).

Tunaweza kutamatisha kwamba Agano Jipya inazungumza kuhusu hali yetu ya dhambi kama "mwili" kwa sababu mwili ni ujasiri wa nafsi. Tabia ya msingi kabisa kuhusu mwili ni kwamba



uwezo wa kiroho kuweza kupata ushindi juu ya mambo haya.

Wakati sheria inaingia katika maisha yetu – labda kwa kushika sheria au kwa kuchagua kutenda mema – dhambi inahuika tena, nasi tunakufa. 1 Wakorintho 15:59 inatuambia kwamba dhambi inapata nguvu na kuwa hai kutokana na majaribio yetu ya kudumisha sheria kwa nia zetu. Kufikia sasa tumekumbana na mauti mara nyingi kiasi ambacho tunaweza kuelezea jinsi yalivyo. Inakuwa namna hii: tunaamua kufuata amri au tunachagua kutenda mema katika eneo fulani. Dhambi, ambayo ni nia kuwa tunajitosheleza na kufikiri kwamba tunajua kila kitu, inakuwa hai tena. Hii inasababisha bidii zetu za kiroho zishindwe. Hukumu inaingia ikifuatwa na hali ya kufinyiliwa katika mawazo – ambayo inasababisha tujisikie kuwa hatustahili. Maisha kama haya yanaweza kutambulika vizuri kama "mauti". Kwa hivyo, uhuru kutoka kwa sheria ni uhuru kutoka kwa "mauti". Tunayatambua hayo mauti kwa ujuzi, kwa sababu tumeishi miaka mingi chini ya utawala wake bila kutambua shida yetu na jambo ambalo tungefanya ili tubadilike na tupate ushindi katika maisha yetu. Tumshukuru Mungu kwa kuwa kuna njia ya kutokea.

Kwa sababu ya umoja wetu na Kristo katika kusulubishwa, tunaweza kuwa huru kutoka kwa kuishi chini ya sheria. Kifungu muhimu kinachoeleza uhuru wetu kutoka kwa sheria ni Warumi 7:4: *"Kadhalika, ndugu zangu,ninyi pia mmeifia torati, kwa njia ya mwili wa Kristo, mpate kuwa mali ya mwingine, yeye aliye fufuka katika wafu, kusudi tumzalie Mungu matunda".* Hii inazungumzia kuhusu kusulubishwa, kuzikwa na kufufuliwa kwetu, mambo ambayo tulikwisha kuona Paulo anayaunda katika Warumi 6:3-13. Hivyo basi, wote wanaoishi chini ya sheria pia waishi katika mwili. Lakini tunapopata ujuzi katika kusulubishwa kwa mwili wetu, basi tunakuwa huru kutoka kwa kuishi chini ya sheria.

Katika Warumi 7:3, Paulo anatukumbusha kwamba, mwanamke anakuwa huru kutoka kwa mume wake, wakati mume anapofariki. Kisha katika msitari wa 4, anatuarifu kwamba, tunawekwa huru kutoka kwa sheria katika kusulubishwa kwetu, ili tuweze kuolewa na mwingine, ambaye ni Bwana Yesu Kristo. Wazo la utukufu! Wengi wetu tumesikia kwa miaka mingi kwamba Kanisa ni bibi harusi wa Kristo. Hapa, Maandiko yanatuarifu kwamba, kila Mkristo anaweza kuishi maisha yake kibinafsi kama bibi harusi wa Kristo. Lakini, hatutaishi katika mahali hapo pa juu mpaka tutakapoacha sheria zetu wenyewe na tuchague kuhusiana naye kama Bwana Harusi wetu. Tutaishije maisha ya unyenyekevu chini ya Bwana Harusi wetu, wakati ambapo tumeshaweka malengo yetu maishani na jinsi ambavyo tutayafikia?

Unaweza kuuliza, "Itakuwaje kuhusu amri za Maandiko – kwani haitupasi kuzitii?" Jibu moja kwa swali hili ni, "Tutakapomwitika Bwana kama Bwana Harusi wetu, tutakuwa kwa uhakika, tumetimiza amri za Maandiko. Hebu fikiri kuhusu huduma za Roho Mtakatifu katika maisha yetu: anatuongoza kushuhudia, anatuongoza katika kweli yote – hii inamaanisha, kati ya mambo mengine mengi, kwamba anatuhimiza kuchambua Biblia. Kasha anatuongoza katika maombi. Pia anatujaza kwa upendo, imani na uaminifu. Kwa ufupi, tunapotembea katika Roho, tutatembea katika makubaliano na amri za Biblia.

Je, hii inamaanisha kwamba hatuhitaji kusoma Biblia zetu? La, haimaanishi hivyo. Roho Mtakatifu, kwa sababu anatuongoza katika kweli yote, ataendelea kutuweka katika kusoma na kuchambua Biblia zetu. Tunapotembea katika Roho, ufahamu wetu wa Biblia na kuielewa kutaongezeka. Hata waamini wengine, watafanyika kuwa wanafunzi wa Maandiko, kwa mara ya

Sababu ni kwamba, wakati mwili (asili ya dhambi) unapoweka sheria, huwa haupendezwi wakati wengine wanakosa kufuata hizo sheria. Pili, ijapokuwa kuna makusudi ya kutenda mambo mazuri kwa anayeishi chini ya sheria, inakuwa ni vigumu kwake kumtumtumikia Mungu. Katika kitabu cha Warumi 8:6-7, Paulo anatangaza kwamba, *"Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti… kwa maana haitii sheria ya Mungu."* Tunapokuwa na nia kwamba sisi tuna hekima kumliko Mungu, basi hatutasikiza yale ambayo Bwana anapendekeza katika maisha yetu. Na hivyo tutajipata tukikaidi mapenzi ya Mungu.

Mmojawapo ya matamshi makubwa zaidi katika Maandiko, ni ushuda wa Paulo katika Warumi 7:9, mahali ambako anazungumzia kuhusu kurudi tena kuwa chini ya sheria baada ya kuwa Mkristo. Anasema, *"Nami nalikuwa hai hapo kwanza bila sheria; ila ilipokuja ile amri, dhambi ilihuika, nami nikafa."* Kwa Paulo, kuishi kulingana na sheria inamaanisha kifo.

Wengine wanaamini kwamba huu ushuhuda unazungumzia maisha ya Paulo kabla ya kuwa Mkristo. Ila mjadala wa hichi kifungu unaonyesha kwamba tayari alikuwa mwamini. Ufunguo wa kuelewa ushuhuda wa Paulo (kwamba alikuwa Mkristo) ni kuwa, hakuna wakati alikuwa anaishi "bila sheria" kabla ya wokovu wake. Matamshi yake katika Wafilipi 3:5 yanadai kuwa alikuwa "Mwebrania wa Waebrania". Hii inaonyesha kwamba aliishi akifuata sheria kutoka utotoni mwake. Jambo lingine la kuzingatia ni maneno yake kwamba "dhambi ilihuika" au ilikuwa hai. Hii ingegusia kwamba dhambi ilikuwa imetoka mamlakani hapo awali, lakini ikarudi kuwa hai tena.

Watu wengi wanaokuja kwa Kristo wakiwa watu wazima, wako na ushuhuda kama huu uliofafanuliwa. Kwa kipindi cha wakati baada ya kumpokea Kristo, maisha yalikuwa yenye furaha, wakitembea pamoja na Mungu, bila ya mawazo yeyote kuhusu kuishi kulingana na sheria. Lakini baada ya muda, marafaki walio-watakia mema, waliwafundisha kwamba wanahitaji kujipatia nidhamu ya kuweka vipindi vya wakati vya kusali pamoja na kuchambua Biblia. Majaribio hayo ya nidhamu yaliwaweka chini ya sheria, kwa sababu yaliweka mzigo wa maisha yao juu yao wenyewe. Sasa inawapasa kutenda mambo kwa mtindo fulani.
Paulo alirudi namna gani katika kuishi chini ya sheria baada ya kuwa muumini anayeishi kwa Neema? Hatujui kwa uhakika, lakini tunaweza kupata ishara katika matamshi yake kwamba tamaa ilimjaa wakati alikumbushwa kuhusu amri inayokataza tamaa. Kuna uwezakano aliwaza, "Ni lazima nijitahidi sana ili nisiwe na tamaa sasa nilivyo Mkristo, kama ilivyokuwa nilipokuwa Mfarisayo." Sheria ikaingia! Sheria inapokuja, mzigo wa ushindi katika Kristo sasa ulikuwa juu yake. Ujasiri wa kibinafsi ukarudi. Dhambi ikarudi. Mauti yalikuwa karibu.

Paulo anamaanisha nini anapotaja mauti? Hakufa kimwili. Hakupoteza wokovu wake. Anamaanisha hali ya mawazo katika hisia na roho ambayo inaweza kufafanuliwa vizuri zaidi kwa neno "mauti". Ni hali ya mawazo ambayo Paulo anaifafanua katika Warumi 7:15: *"Maana sijui nifanyalo, kwa sababu lile nilipendalo, silitendi; bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda."* Je, haya yanakukumbusha mtu yeyote unayemjua? Nafikiri sisi sote tumekumbana na mauti ambayo Paulo alikumbana nayo. Tunaweza kuwa na tamanio ndani yetu ya kutenda mambo ambayo tunajua kwamba tunastahili kuyafanya; kupenda adui zetu, kuwasamehe wanaotukosea, kuhudumu kwa njia nyingi, kuwashuhudia wasioamnini, nk. Lakini haijalishi kiasi cha tamanio tulichonacho na bidii tunayoweka katika kutenda mambo haya, sisi hatuna uwezo wa kuyatenda kikamilifu. Tunaweza kujaribu, lakini hatuna uwezo wa kufanikiwa. Kushindwa kwetu ni kuishi katika mauti. Labda tunajichukia kwa sababu ya mishutuko yetu ya hasira, uwoga, wivu, kukosa uvumilivu, kukosa upendo, na kukosa ujasiri – pamoja na matendo mengine mengi ya mwili. Lakini, hatuna



huwa tunafikiri kuwa sisi tu wenye hekima na kwamba tunajua kila kitu. Ijapokuwa mara nyingi hili huwa si wazo tunalolifahamu, lakini kwa udhahiri linapatikana ndani yetu sisi sote.

Hii shida yetu ya ugonjwa wa kiroho ililetwa na baba wetu wa kiasili, Adamu, wakati alipokula tunda la mti aliokuwa amekanywa. Ijapokuwa sisi hatukuwepo pale Adamu alipoharibiwa, hata sisi pia tuliharibiwa kwa sababu yeye ndiye kichwa cha kizazi cha kiasili. Hivyo basi, hii hali ya dhambi inapitishwa kwetu katika hali ya kutunga mimba na kuzaa wakati tunapozaliwa katika kizazi cha Adamu.

## SURA YA NNE: KUSULUBISHWA, KUZIKWA, KUFUFUKA NA KUKETISHWA PAMOJA NA KRISTO

Tayari tumekwisha kuona kwamba tulipoingia katika kizazi cha Yesu, tulisulubishwa, kuzikwa na kufufuliwa. Ni hivyo kwa sababu Bwana wetu alisulubishwa kama "Adamu wa Mwisho" – kichwa cha kizazi cha kiroho. Maandiko yanatuambia mambo manne kuhusu kusulubishwa kwetu.

Jambo la kwanza ni kwamba mtu wetu wa Kale amesulubishwa. Paulo anaandika, *"Mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye"* (Warumi 6:6). Utu wetu wa kale ni aina ya utu tulionao kutokana na kuzaliwa kwetu mara ya kwanza – katika kizazi cha Adamu. Hata hivyo ni lazima ujue kwamba kusulubishwa kwa mtu wetu wa kale hakumaanishi kuangamizwa kabisa kwa mtu wetu wa kale. Ikiwa hiyo ingekuwa kweli, Wakristo wasingelikuwa na tatizo la dhambi. Hata hivyo, ijapokuwa mtu wetu wa kale hajaondolewa kabisa, inamaanisha kwamba anaweza kuondolewa katika mamlaka. Kama matokeo, tunaweza kupata ongezeko la uhuru kutoka kwake kwa kuishi katika umoja wetu na Kristo.

Warumi 6:2 inataja jambo la pili kuhusu kusulubishwa kwetu – kwamba tumeifia dhambi. *"Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije katika dhambi?"* Warumi 6:10 pia inatuambia kuwa Yesu *"aliifia dhambi"*. Na mara baada ya tamko la Paulo kwamba Yesu aliifia dhambi, anatuamuru tujitambue kwamba nasi pia tumeifia dhambi. Wakati tumefia jambo, basi tumetanganishwa nalo.

Jambo la tatu kuhusu kusulubiwa kwetu ni kwamba tumesulubishwa kwa ulimwengu. Paulo anashuhudia: *"Lakini mimi, hasha, nisione fahari juu ya kitu chochote ila msalaba wa Bwana Kristo, ambao kwa huo ulimwengu umesulubishwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu"* (Wagalatia 6:14). Hapa, hili neno ulimwengu, linazungumzia nini? Ulimwengu unajumulisha wale wote ambao hawatembei katika Roho. Kwa hivyo Wakristo wanaoishi katika mwili, na watu wote ambao hawajaokoka, wote ni wa ulimwengu. "Watu wa ulimwengu" wanaweza pia kuwa watu wa karibu sana kwako. Ijapokuwa wanaweza kuonekana kuwa ni watu wazuri, huenda wakawa wanakuongoza mbali kutoka kwa mapenzi ya Bwana. Hivyo basi, kuna uwezekano kwamba tunashawishiwa na ulimwengu zaidi ya vile tujuavyo.

Jambo la nne tunalojifunza kuhusu kusulubishwa kwetu ni kwamba tumesulubishwa kwa kuishi kulingana na amri. Kuna sababu kuu ya kusherekea tunapotambua kwamba tumefia kuishi chini ya amri. Katika Warumi 7:14, Paulo anatuonyesha ukweli huu kwa kutumia mfano rahisi wa ndoa kati ya mume na mke. Wakati mume anapokufa, mke anakuwa huru kuolewa tena. Hayuko tena chini ya mamlaka ya yule bwana ila yuko huru kuolewa na mume mwingine. Katika matumizi ya Paulo, Mkristo ndiye mke. Mabwana wawili ni amri na Kristo. Kinachomweka mke huru ni mauti yake mwenyewe. Mfano unatuonyesha kwamba sisi kama waaminio tumeifia amri kupitia kwa kusulubishwa kwetu na Kristo. Hii inatuwezesha kuwa huru kutokana na kifungo cha amri. Na huu uhusiano mpya wa ndoa na Kristo akiwa mume wetu humzalia Mungu matunda.

Wakati mwelekeo wetu kuishi maisha ya Kikristo ni ule wa kuweka sheria (au kujaribu kushikilia amri), basi tunajiwekelea mzigo sisi wenyewe. Nia yetu ni kuwa "nitafanya haya" au "sitafanya yale". Mauti yetu kuifia amri, basi ni uhuru kutokana na jitihada kudumisha amri za Bibilia katika



## SURA YA KUMI NA MOJA: UHURU KUTOKA KWA SHERIA

Katika Warumi 7:7-25, Paulo anatoa ushuhuda wake kuhusu jitihada zake za kuishi katika sheria na jinsi zilivyoishia katika mfano wa mauti ya kiroho iliyomsukuma kwa Mungu ili apate neema. Anaanza ushuhuda wake kwa kutuonyesha katika Warumi 7:1-6 jinsi tunavyo weza kupokea uhuru kutoka kwa sheria kwa kutambua umoja wetu na Kristo. Kifungu hichi kuhusu sheria hakijapata kuzingatiwa kikamilifu na Wakristo. Ijapokuwa ni lazima tuelewe kuhusika kwetu pamoja na uhuru wetu kutoka kwa sheria, ikiwa tutakumbana na uzima tele tele. Uhuru wetu kutoka kwa sheria ni wa umuhimu zaidi kuliko Wakristo wengine wanavyotambua.

*"Mmeokolewa kwa neema kupitia kwa imani"* (Waefeso 2:8). Sote tunakifahamu kifungu hichi na waumini watasimama katika ukweli wake katika umilele wote. Tunajua kwamba wokovu haujawahi na wala hautawahi kupeanwa kwa yeyote kwa sababu ya kutimiza sheria. Hata hivyo, baada ya wokovu, waumini wengi wanakuwa wana sheria katika azimio lao la kuishi maisha ya wokovu pasi na kutambua makosa yao.

Paulo anazungumza kuhusu huku kuchanganyikiwa katika Wagalatia 3:2. *"Mlipokea Roho kwa kutimiza sheria au kwa kuamini mlichosikia? Kwani mmekua wapumbavu? Baada ya kuanza katika Roho, je sasa mnajaribu kuafikia malengo yenu kwa bidii zenu?"* ijapokuwa waliokolewa kwa imani, sasa wanajaribu kuishi maisha yao ya Kikristo kwa juhudi zao wenyewe.
Mfano wa kawaida wa Mkristo anayeishi maisha ya kisheria ni kama mtu ambaye anasoma Amri Kumi kila asubuhi akiwa na mpango wa kuzitimiza maishani mwake mchana kutwa. Wengi wetu hatujaribu kufanya hivyo – kwa sababu tunajua haiwezekani! Hata hivyo, wengi wetu tumemwahidi Mungu kwamba tutaomba au kusoma Bibilia zetu kwa kiwango fulani cha wakati kila siku. Na katika kufanya ahadi hizi, tunajiweka chini ya sheria kiasi ambacho ni kama tunajaribu kutimiza Amri Kumi.

Sheria ambazo tunajaribu kufuata, huenda zilitoka kwa mtu ambaye alitufundisha neno la Mungu au kwa Mkristo mwingine aliyeamini kwamba anatusaidia kuishi maisha ya Kikristo. Haijalishi hizo sheria zilitoka wapi. Kinachojalisha ni kwamba, tunajaribu kutii sheria kwa nguvu zetu wenyewe, na hii ni jitihahada ya asili yetu ya dhambi na haijalishi hayo matendo yatakuwa mazuri kiasi gani. Katika Warumi 7:21, Paulo anatoa ufunuo kwamba, sisi tuna hatia ya kuishi chini ya sheria hata kama matendo yetu ni hatua zaidi ya kuchagua kutenda mema. Tunafanya tangazo: "nitafanya jambo hili", "sitafanya jambo lile." Kwa bahati mbaya, waumini wengi wanaishi chini ya sheria hizi bila hata kujua. Tunapojaribu kumtumikia Bwana katika nguvu zetu wenyewe, tutakuwa na hatia ya kutenda kazi za mwili.

Tunapokuwa na uhuru kutoka kwa sheria, pia tunakuwa na uhuru kutoka kwa asili ya dhambi. Na hii itatuweka huru kutoka kwa dhambi za kufisha. Baadhi ya hizi zinatajwa katika Wagalatia 5:19-21: *"…Matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo."*

Tuchunguze mambo mengine mawili yanayotokana na kuishi chini ya sheria. Kwanza, wale ambao wanashikilia sheria kwa nguvu zaidi ndio ambao wanakuwa na nia za kuhukumu wengine.

ulimwengu kama vile tunavyo jitambua kuwa tumekufa kwa dhambi na tuko hai kwa Mungu. Tutakapo chagua kuwa huru kutoka kwa ulimwengu, Mungu atakuwa mwaminifu kutupatia uhuru huu hatua kwa hatua. Jukumu letu hata hivyo, ni kukabili kwa upesi na umakini sehemu za udunia katika maisha yetu ambayo Roho Mtakatifu atatufunulia. Lakini inatupasa kufanya hivyo kwa upesi. Tukikawia, itakuwa vigumu zaidi kuvua sehemu za udunia zinazo tupunguzia nguvu za kiroho. Tukiendelea kukawia katika kukabili mambo haya, basi Roho Mtakatifu ataugua na kuzimika.



nguvu zetu wenyewe. Tunao uhuru kutokana na kutimiza sheria zilizowekwa na mwanadamu, uhuru kutoka kwa jitihada ya kujaribu kumfurahisha Yesu na hata uhuru kutoka kwa kujaribu kutenda mema. Mauti yetu kwa sheria ndio uhuru kutokana na mwili pamoja na hitilafu zote za uwezo wake.

Sisi sio tu kwamba tunasulubishwa pamoja na Kristo, lakini Maandiko yanatueleza kwamba pia tunazikwa pamoja naye. Warumi 6:4 inasema, *"basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake."* Kuzikwa kwetu kunatuongeza ushindi muhimu juu ya mtu wetu wa kale – amesulubishwa na pia amezikwa. Sababu pekee ambayo Maandiko yanatupatia kuhusu kuzikwa kwetu ni kwamba ni maandalizi ya ufufuo wetu. Warumi 6:4 inasema, *"basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."*

Tunazikwa ili kwamba tufufuliwe. Hivyo basi, majadiliano yeyote kuhusu kuzikwa kwetu kunatutanguliza katika uchambuzi wa somo la ufufuo wetu. Katika Warumi 6:5, Paulo anaandika, *"kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake."* Ujumbe wa Warumi 5:4-5 ni kwamba waaminio wana fursa na uweza wa kutembea katika upya wa uzima kwa sababu wamefufuliwa kama vile Bwana wao alivyofufuka. Ufufuo wetu na mauti yetu ni kama mauti na ufufuo wa Kristo, lakini Wake ulikuwa wa kimwili na wetu ni wa kiroho. Roho wa Mungu alikuja kuishi ndani yetu wakati wa wokovu wetu. Ametufanya kuwa hai katika Kristo.

Ufufuo wa kiroho wa waaminio wote una ngazi tatu. Tumefanywa kuwa hai, tukainuliwa na kuketishwa katika maeneo ya mbinguni. Wakati Kristo alifufuliwa kutoka kwa wafu, sio tu kwamba alifufuliwa, lakini pia aliinuliwa na kuketishwa katika maeneo ya mbinguni. Kwa hivyo ni lazima tuelewe maana kwamba tumeketishwa pamoja na Kristo. Tunawekwa pale pamoja naye katika dakika ya wokovu wetu wakati tunapoingizwa katika umoja na Kristo.

Sehemu hii ya ujumbe kuhusu umoja wetu na Kristo ndiyo ambayo huonekana kuwa ngumu zaidi ya kueleweka. Wakati Paulo anawaombea waumini walio Efeso, anaomba kwamba watakamata ukuu wa uwezo unaopatikana kwa ajili ya wote walioamini (Waefeso 1:19-20). Hizo ndizo nguvu ambazo zilidhihirika ndani ya Yesu na zinapatikana tu kwa wale wanaoendelea kuishi maisha ya kumtegemea Mungu. Hivi ndivyo Paulo anavyoifafanua, *"na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; akavitia vitu vyote chini ya miguu yake…"* (Waefeso 1:19-20). Kwa sababu waaminio wako katika umoja na Kristo, wanaweza kupata maisha ya nguvu za ufufuo na kuketishwa pamoja naye katika nafasi ya utawala Wake na mamlaka.

**SURA YA TANO: TUTAWEZAJE KUIPOKEA HII NEEMA?**

Hata waumini wasioelelewa kuhusu umoja wao na Kristo wanashiriki baadhi ya faida za kusulubishwa, kuzikwa na kufufuka kwao. Hata hivyo, hatutaweza kushiriki kikamilifu mambo haya mpaka tutakapofuata yale tuliyoonyeshwa katika Maandiko. Kama vile tulivyopokea wokovu wetu kwa kuelimishwa na halafu kuamini, vile vile, hivyo ndivyo tunavyoshiriki kikamilifu kusulubishwa kwetu, kuzikwa na kufufuliwa. Hatua za kushiriki mambo haya zimetolewa katika Warumi 6:3-13.

Jambo la kwanza ambalo ni lazima tulizingatie ni jukumu letu la kuamini kwamba tayari tumesulubishwa, kuzikwa na kufufuliwa. Kuna amri mbili kuhusu swala hili. Ya kwanza ni: *"Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu"* (Warumi 6:11). Kuamini kwetu kwamba tumefia dhambi na tuko hai kwa Mungu si ahadi kwa Mungu kwamba hatutatenda dhambi tena, wala sio kutubu kwa dhambi fulani ambayo tumeitenda. Hii ni kuamini tu kwa urahisi kwamba tumefia dhambi na kuwa tuko hai kwa Mungu. Tizama pia kwamba hii ni amri. Hivyo basi, ikiwa hatuamini kuwa jambo hili ni kweli, basi tunaishi katika uasi. Amri ya pili ya imani iko katika kifungu cha 13, *"…bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa…"* ikiwa tutachukua mjadala wa kifungu chote, tunaweza kuona kwamba Paulo anasema kuwa tujitoe au kujitiisha wenyewe kwa Mungu kama wale waliosulubishwa, wakazikwa na wakafufuka.

Amri ya Paulo ya "jihesabuni" au kuaamini (kf. 11) ni amri ambayo inahitaji uendelezi wa matendo kwa upande wetu. Inatupasa kuamini kila wakati kwa siku kwamba tumefia dhambi na tuko hai kwa Mungu na tunatakiwa tuendelee kujitiisha wenyewe kwa Mungu tunapotii hizi amri.
Watu wengine wamepeana picha kwamba kutii amri hizi ni tendo la wakati mmoja pekee. Ikiwa hiyo ingekuwa kweli, basi wakati mtu anapoamini na kuchagua umoja wake na Kristo, angeweza kuishi katika ushindi siku zake zote zilizosalia hapa duniani. Lakini kwa kuwa hiyo si kweli, picha hiyo ya uongo kamwe haiambatani na Maandiko na wala haisidii.

Katika Warumi 8:2 Paulo anaandika: *"Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti."* Hii inatuambia kwamba Roho Mtakatifu hutenda kazi katika maisha ya waumini wote kulingana na sheria fulani. Sheria hiyo ni kutupatia uzima tele tele kupitia kwa umoja wetu na Kristo. Hivyo basi, Roho Mtakatifu atatukumbusha kila wakati wa siku kwamba tumeifia dhambi na tuko hai kwa Mungu.

Katika Warumi 6:16, Paulo anatuarifu kwamba tunafanyika kuwa watumwa wa vile vitu tunavyovitenda mara tena na tena. Basi tunapoamini tena na tena kwamba tumeifia dhambi na tuko hai kwa Mungu, hatimaye tutakuwa watumwa wa imani hiyo. Kwa maneno mengine, itachukua utawala wa maisha yetu. Hata hivyo, hii ni hatua na itagharimu wakati.

Hivi ndivyo inavyofanya kazi: Katika mwanzo wa siku, Roho Mtakatifu hutukumbusha kuhusu kusulubishwa, kuzikwa na kufufuka kwetu. Tunaitikia kwa kukubaliana kwamba mambo hayo ni ya kweli kutuhusu. Kisha, kadri siku inavyoendelea, anatukumbusha kwa upole. Pale mwanzo tunaweza kuenda masaa mengi kwa wakati mmoja bila ya kumtambua Mungu na umoja wetu na Kristo. Lakini, kwa wakati, tunaunda tabia ya kuamini kwamba sisi tumeifia dhambi na tuko hai kwa Mungu. Kuamini kwamba tayari tumesulubishwa inamaanisha kuwa tunaamini kwamba tumeifia dhambi; mtu wetu wa kale amesulubishwa; tumesulubishwa kwa ulimwengu; na



**SURA YA KUMI: UHURU KUTOKA KWA ULIMWENGU**

Paulo anatuhimiza, *"msifananishwe tena kwa mfano wa ulimwengu huu, lakini mkabadilishwe kwa kufanywa upya katika nia zenu"* (Warumi 12:2). Hili andiko linatuonyesha kwamba sisi sote tunayo tamanio ya kufanana (ama kuiga) na kile watu wengine wanafanya. Paulo alitambua tabia yake ya kujaribu kujifananisha na aliikiri. *"Naomba kwamba nisiwahi kujivuna isipokua katika msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambapo ulimwengu wote umesulubishwa kwangu na mimi kwa ulimwengu"* (Wagalatia 6:14).

Waumini wote ni lazima watambue tamaa yao ya kutaka kufanana na ulimwengu. Ni lazima tutambue maeneo ambayo huenda ikawa tumesha fananishwa na ulimwengu. Wengi wetu hufikiria kwamba ulimwengu ni wale wasioamini na wamemkataa Bwana wetu – wale wanaoshi katika dhambi iliyo wazi kwa Mungu. Lakini, inatupasa kuona ulimwengu kama wote wanaoishi chini ya utawala wa Shetani na wa mwili hata ikiwa ni waumini au hawaamini. Kwa maneno mengine, yeyote ambaye hatembei katika Roho.

Inawezekana kuwa wale wanaotushawishi zaidi wako na udunia ndani yao. Hata wanaweza kuwa ni viongozi Wakristo tunao wajua. Lakini wako na udunia kwa sababu wameshawishiwa na Shetani, mwili na ulimwengu ili wapokee mitindo ya maisha iliyo kinyume na yale ambayo maandiko yanatuambia. Na huenda hata wasijue kuwa wanakubaliana na filosofia za ulimwengu.

Tunahitaji kuweka njia zetu za kutazama maisha kando na ukweli wa Maandiko. Mahali jambo halikubaliani na Andiko, hilo ni kosa na ni filosofia ya ulimwengu. Kama saratani hatari iliyofichika, filosofia za kidunia zilizofichika kwetu huenda zikawa zinatutafuna katika maisha yetu ya kiroho na katika utenda kazi wetu.

Agano Jipya inatufundisha tuishi maisha yetu dakika kwa dakika katika hali ya kumtegemea Mungu kikamilifu kwa mambo yote. Hata hivyo, tutajipata tukitumainia nguvu zetu na hekima kwa mda mwingi zaidi. Warumi 1:17 inasema, *"Wenye haki wataishi kwa imani."* Waebrania 11:6 inatuambia; *"lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu."* Mtu anayeishi kwa imani humtumainia Mungu katika kila dakika ya maisha yake. Kwa imani kama hiyo, tunamtegemea Mungu kutuonyesha jambo la kufanya kila wakati. Mtu mwenye imani kama hii ndiye anayepatikana kutumika mbele za Mungu. Warumi 12:1 inatuamuru, *"Toeni miili yenu kama dhabihu iliyo hai."* Warumi 6:13 inasema, *"Toa sehemu za mwili wako Kwake kama vifaa vya haki."* Tunapo mtumainia Mungu kutuonyesha yale ya kufanya kila wakati, na kuitikia mwongozo Wake, basi tutakuwa tumepatikana mbele Zake kikamilifu.

Ushuhuda wa Paulo katika Wagalatia 6:14 unatuonyesha awamu ya kina zaidi ya msalaba kuliko ile ambayo wengi wetu wametambua au hata kutumia. Tunahitaji kuchunguza jinsi tunaweza kupokea uhuru kutoka kwa ulimwengu kwa kusulubishwa katika kuamini na hata kuchagua.

Natuwaze jinsi ulimwengu ulivyosulubishwa kwetu na sisi tulivyo sulubishwa kwa ulimwengu. Bwana ni mwaminifu na atatufunulia sura za udunia zilizofichika ndani yetu ikiwa zipo. Baadhi ya funuo za udunia huenda zikawa zenye uchungu mwingi. Huenda tukashawishika kuachana na tabia ambazo zimeundika kwa miaka mingi. Ushindi kinyume na tabia hizi huenda ikaonekana kana kwamba haiwezekani. Lakini hiyo si kweli.

Tunastahili kutambua kuwa ulimwengu umesulubishwa kwetu na sisi tusulubishwe kwa

Ni lazima tukumbuke kwamba hakuna kitu kama kufikia mahali ambako hatutendi dhambi tena katika maisha haya. Hata hivyo, tunaweza kupata uhuru kutoka kwa dhambi ambayo ni hatua kubwa kutoka kwa maisha ya kulemewa ambayo wengi wameyakubali kama jambo la kawaida katika maisha ya Kikristo.

Natukubali kwa imani ya kwamba kwa wakati, tunaweza kuwa huru kutoka kwa dhambi inayotufunga pamoja na adhari zake. Dhambi zetu zimetufanya kuishi katika hali ambapo hatutamani kuishi, hali ambayo ni duni sana ikilinganishwa na yale Mungu aliyotukusudia – uzima tele tele. Tunaweza kupata ujasiri kwamba tutaweza kupiga hatua katika kupokea uhuru wetu kutoka kwa dhambi. Lakini, ili haya yatendeke, ni lazima tuendelee kuamini na kutambua umoja wetu na Kristo katika kusulubishwa, kuzikwa na kufufuka.



tumesulubishwa kwa sheria.

Uhuru wetu kutoka kwa kifungo cha hali yetu ya dhambi pia unadhihirishwa katika ukweli kwamba mtu wetu wa kale amesulubishwa. Mwili wetu na yote uliozalisha katika maisha yetu umesulubishwa. Wazo hili linatupatia ushindi mara mbili juu ya hali yetu ya dhambi. Tumekufa kufikia mahali ambako hali yetu ya dhambi inahusika, na hali yetu ya dhambi imesulubishwa.

Hivyo basi, tunaweza kuamini kwamba, sio lazima tuendelee kutenda dhambi kisha tuwe wa kufadhaika. Hatusemi kwamba tunaamini kwamba hatutatenda dhambi tena. Ila ni kuamini kwamba *hatuhitaji kutenda dhambi.*

Unaweza kuchukua hiyo kanuni ya imani na kuifanyisha kazi hivi sasa. Mshukuru Bwana kwamba hauhitaji tena kuwa chini ya utawala wa dhambi. Hauhitaji tena kujawa na hofu, wivu, hasira, uchungu moyoni, wasiwasi, kujawa na tamaa au kutumishwa na dhambi yeyote ambayo imesababisha fedheha maishani mwako.

Pamoja na mtu wetu wa kale kuwa amesulubishwa, pia amezikwa. Huku kuzikwa ni matayarisho ya kufufuka. Tumesulubishwa na kuzikwa ili kwamba tuweze kufufuliwa na kuwekwa kiroho katika uwepo wa Baba. Katika Waefeso 2:4-7, tunaambiwa kuwa Roho Mtakatifu amekuja kuishi ndani yetu. Tumefufuliwa kutoka kwa wafu na tumeketishwa katika maeneo ya mbinguni. "*Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho…*" (kf. 6). Hii huonekana ikiwa ngumu sana kwa waamini wengine kuweza kuelewa. Pengine ni ngumu kwa sababu inaonekana kuwa ni maisha yenye utukufu mwingi kiasi kwamba hatuwezi kuwaza yeyote akiishi katika uwepo wa Mungu. Au pengine tunaamini kwamba hatustahili kupokea baraka kama hizo. Lakini, ni lazima tukumbuke kwamba kila kitu kuhusu wokovu wetu ni zawadi kutoka kwa Mungu. Hatukustahili! Basi tuchukue hatua ya imani na tumshukuru Mungu kwamba tumeketishwa pamoja na Kristo katika maeneo ya mbinguni.

Majadiliano haya yote kuhusu umoja wetu na Kristo huenda yakawa yamekusababisha kushangaa, "Ikiwa tayari tumesulubishwa, kuzikwa na kufufuka, ni kwa nini basi tuamini mambo haya kuwa kweli kutuhusu ili kwamba tuweze kuyashiriki?" Lakini ukweli ni kwamba, kuna mambo katika maisha ya Kikristo ambayo hatutayashiriki mpaka tutakapoamini kwamba ni ya kweli!

Msamaha wa dhambi zetu ni mfano mzuri wa hii sheria ya kiroho. Je, umeshawahi kuungama dhambi, zaidi ya mara moja, ambayo ulikuwa umeitenda? Dhambi zingine huenda ikawa uliziungama mara nyingi. Lakini, je, ulisamehewa? 1 Yohana 1:9 inatuambia, "*Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.*" Sasa ikiwa ulisamehewa mara moja, mbona uliendelea kuikiri dhamba ile mara tena na tena? Uwezekano ni kwamba huenda ikawa hukuwa umehisi kuwa umesamehewa. Hukuwa umeamini kwa uhakika kwamba Mungu angekusamehe ikiwa tu ungeungama dhambi ile. Watu wengine huendelea kuishi na hisia za hatia kwa miaka mingi, kwa sababu hawaamini kwamba Mungu amesamehe dhambi fulani ambayo walikuwa wameitenda hapo kale. Kwa hivyo, hawashiriki msamaha ijapokuwa msamaha ni hakika kwao. Katika njia hiyo, tutaweza kushiriki kusulubishwa, kuzikwa na kufufuka kwetu wakati tu *tutakapoamini* kwamba tayari tumeshasulubishwa, tukazikwa na tukafufuliwa.

**SURA YA SITA: AMRI NNE KATIKA WARUMI 6:12-13**

Inawezekana tumeamini kwa miaka mingi kuwa tumesulubishwa, kuzikwa na kufufuka pamoja na Kristo, lakini maisha yetu hayajabadilika. Basi ni lazima tuongeze katika kanuni yetu ya imani, tendo la chaguo. Tunapoelewa, kuamini na kuchagua umoja wetu na Kristo, tutaanza kupitia uzima tele tele ambao Mungu ametuwekea. Kuna amri nne katika Warumi 6:12-13 ambazo zinatueleza jinsi ya kufanya chaguo hili kila siku.

Ya kwanza inasema, *"Msiruhusu dhambi itawale miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake"* (kf.12). "Dhambi" hapa inazungumza kuhusu nia zetu za kufikiri kwamba tunajua kila kitu. Kwamba Paulo angetoa amri kama hiyo, inaonyesha kwamba nia hii itaendelea kutafuta kuitawala miili yetu. Tunahitaji kuendelea kujilinda. Na ulinzi wetu ni katika kutekeleza uweza wetu wa uchaguzi wa "Kutoruhusu dhambi kutawala". Inatupasa kuchagua kila wakati, kutoishi katika mawazo yetu na hekima zetu. Inatupasa kuacha kuamua yale tunatakikana kufanya au yale watu wengine wanatakikana kufanya. Na inatupasa kuacha kuamua yale ambayo tunafikiri ni lazima Bwana afanye! Paulo anasema kwamba, wakati dhambi inatawala ndani ya miili yetu tunazingatia miili yetu zaidi nazo zinatutawala.

Amri ya pili inasema, *"Wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi"* (kf. 13). Hii amri inafanana na ile ya kwanza ingawa iko makini zaidi. Amri ya kifungu cha 12 inazungumza kuhusu mwili wote. Hii inazungumza kuhusu viungo vya mwili. Kama mfano wa yale Paulo anazungumzia, fikiria kuhusu uwezo wa kuongea. Mara mia na mia tunaongea kila siku. Ila, kulingana na hii amri, hatustahili kujiamulia wenyewe yale ambayo tutaongea. Paulo anashughulikia "viungo vya mwili" katika kifungu hichi badili ya mwili wote ambao alitaja katika kifungu cha 12. Mabadiliko yanamaanisha kwamba watoto wengi wa Mungu wanataka Bwana atawale maisha yao – lakini sio kikamilifu. Wanatamani kuhifadhi sehemu zingine za miili yao au maisha yao, ili wazitawale wenyewe. Kwa sabau hiyo, Paulo anaamuru kwamba tusiache hata sehemu moja ya mwili wetu chini ya utawala wetu wenyewe. Kifungu hichi kinatuonya kwamba, tunapofanya uamuzi wa kutumia sehemu za miili yetu kwa ajili ya makusudi yetu wenyewe, ukosefu wa utakatifu ndio matokeo.

Paulo anatupatia mbadili katika sehemu ya katikati ya kifungu cha 13: *"Bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa."* Hii amri ya tatu inatuonyesha kwamba tunahitaji kuchagua maisha ya umoja na Kristo. Mazoezi ya mapenzi yetu yamewasilishwa katika maneno manne ya kwanza – *"Jitoeni wenyewe kwa Mungu."* Lakini hili si zoezi la mara moja, kwa sababu tutajipata tena tukiyatawala maisha yetu. Halafu pia, tunahitaji kujibu kwa kufanya uamuzi mwingine wa kujipeana kwa Mungu.

Amri ya kujipeana kwa Mungu kama waliofufuka kutoka kwa wafu, huenda ikawa tofauti na mashauri ambayo tumewapa watu ambao tunajaribu kuwasaidia wakue katika maisha yao ya Kikristo. Huenda tuliwatajia kwamba wanahitaji kusoma Biblia na kuomba zaidi. Au labda tuliwaambia wayakabidhi maisha yao upya kwa Bwana na kuwatumikia wengine zaidi. Nasi tukafiria kwamba tunawapa mawaidha mazuri. Huenda ikawa tulijua kwamba inatupasa kupatikana kikamilifu kwa Mungu. Lakini kile ambacho hatukujua, ilikuwa ni kwamba lazima mtu apatikane kikamilifu kwa imani na ufahamu kwamba tumesulubishwa, kuzikwa na kufufuka. Tunapotoa maisha yetu kwa Mungu, kama wale waliofufuka kutoka kwa wafu, tunachukulia kwamba maoni yetu pia yamekufa na kuzikwa. Tamanio letu ni kuishi katika maoni Yake peke yake.



tufanye chaguo la kuyapitia.

Waumini wengine wamefikiri kwa makosa ya kwamba, wanaweza kushinda dhambi kwa kuendelea kukiri dhambi zao (kulingana na kanuni katika 1 Yohana 1:9) na kupokea msamaha. Kufanya hivyo ni muhimu kwa kuwa tunapokea uhuru kutoka kwa uchungu mwingi unaosababishwa na dhambi zetu wakati tunakiri na kupokea msamaha. Hata hivyo, ikiwa hiyo ndiyo yote tunayojua, basi tutaendelea kuwa katika kifungo cha dhambi ambazo zitatufunga kwa siku zetu zote katika hii dunia. Pia ni lazima tukumbuke ya kwamba ni lazima tutambue umoja wetu na Kristo ikiwa tutapata ushindi wa kweli na uhuru kutoka kwa dhambi zetu.

Katika Warumi 6:12, tuliona kwamba Paulo alituamuru tusiruhusu dhambi itawale katika miili yetu. Hii amri inatuonyesha kuwa, nia ya kufikiria kuwa tunajua kila kitu na kwamba tunajitosheleza wenyewe itaendelea kujaribu kutawala maisha yetu. Na katika Warumi 7:17, Paulo anafafanua asili yetu ya dhambi kana kwamba ni mtu mwingine anayeishi ndani yetu na kutusababisha kutenda mambo tunayoyachukia na mambo ambayo hatutamani kuyafanya.

Katika Warumi 6:11-23, anasisitiza uhitaji wetu wa kuendelea kutambua umoja wetu na Kristo katika kusulubishwa, kuzikwa na kufufuka. Ahadi za kifungu hicho zinatuhakikishia kwamba tukiendelea kutambua umoja wetu na Kristo, hatua kwa hatua tutawekwa huru kutoka kwa utawala wa asili ya dhambi. Na matokeo ni kwamba, tutakuwa huru kutoka kwa dhambi zinazotokana na asili ya dhambi.

Kutambua uhuru kutoka kwa dhambi inafananishwa na kuchambua kitunguu. Unatoa ngozi moja na kupata nyingine chini yake. Tunapoanza kutambua uhuru kutoka kwa mambo ambayo yametusabisha huzuni, Roho wa Mungu atatufunulia dhambi zingine ambazo hata hatungeweza kuzijua. Hata hivyo, kwa watu wanao tuzunguka, kuna uwezekano kwamba wameziona ndani yetu kwa miaka mingi! Wakati hizi dhambi zilizofichika zinapofunuliwa, tunahitaji kuanza kuzishughulikia mara moja na kuwekwa huru kutokana nazo. Huenda Bwana akatufunulia dhambi mbili au tatu, ambazo tulikuwa hatuzijui, kwa wakati mmoja. Tunapoendelea kupokea uhuru kutoka kwa hizo, ndipo Atakapotufunulia zingine.

Katika sehemu zingine, kuanzia wakati tunapoanza kukabiliana na dhambi kulingana na hatamu za umoja wetu na Kristo, tunaweza kupokea uhuru kamili kutoka kwa dhambi hiyo. Hata hivyo, sehemu kubwa ya dhambi zetu, zitahitaji kushughulikiwa katika vipindi vya mda mrefu. Dhambi zingine huonekana zikiwa zimekita mizizi katika maisha yetu kuliko zingine. Dhambi hizo zitajitokeza tena na tena.

Wala, tusikate tamaa. Tukiwa na imani kamili katika umoja wetu na Kristo, na katika ahadi za Mungu, basi tuendelee kuamini na kuchagua uhuru kutoka kwa hizo dhambi kaidi. Tusiwahi kukubali kustarehe katika dhambi ya aina yoyote. Kama vile Waisraeli walikosa kuangamiza wakaaji wote wa nchi ya Kaanani ijapukua walikua wamepatiwa amri ya kuwaangamiza, hivyo hivyo watumishi wengine wa Mungu hawajakabiliana na dhambi zao zote.

Bwana aliwaambia wana Israeli wasiotii kwamba, kama wangekataa kuangamiza mataifa mengine yaliyokuwa katika nchi ya Kaanani, basi hayo mataifa yangekuwa "miiba katika mbavu zao" (Waamuzi 2:3). Na tunaona kutoka kwa nakala za historia ya Israeli katika Agano la Kale kwamba unabii huu ulitimia. Katika njia hiyo, dhambi yeyote ambayo tutakosa kuikabili na kupata ushindi dhidi yake, itakuwa mwiba katika mbavu zetu.

**SURA YA TISA: UHURU KUTOKA KWA DHAMBI**

Mlango huu unafundisha habari njema kwamba sio lazima tuendelee kuishi chini ya utawala wa dhambi fulani ambayo inatuletea hisia za kuhukumika na kushindwa. Watu wengine wanaweza kuuliza: "Je, unafundisha kwamba tunaweza kua wakamilifu na tusiwahi kutenda dhambi tena?" Inapasa kutangazwa kwa nguvu kabisa, kwamba ni baada ya kuyawacha maisha haya, ndipo waumini watakapokuwa huru kabisa kutoka kwa dhambi. Hata hivyo, tunaweza kutambua uhuru unao kua kutoka kwa dhambi, na uchungu ambao unasababishwa katika maisha yetu, kabla hatujaenda mbinguni.
Kwa sababu Wakristo wengi wanasikia kuhukumika na wanaamini kuwa dhambi zao ni mbaya zaidi kuliko za watu wengine, inaweza kuwa jambo la kuwatia moyo, tunapo tazama baadhi ya nakala za dhambi katika Bibilia. Vifungu hivi vinaonyesha kwamba sote tuweza kutenda dhambi yoyote ile.

Katika Wakolosai 3:8-10, Paulo anasema, *"Lakini sasa ni lazima mjiepushe na mambo ya aina hii: hasira, gadhabu, uchochezi, uzushi, na lugha chafu kutoka vinywani mwenu. Msidangayane, kwa sababu mmevua utu wenu wa kale pamoja na matendo yake na mmevaa utu mpya, ambao unafanywa upya katika ufahamu katika sura ya Muumba wake."*

Katika kifungu kingine, Paulo anatuambia, *"Lakini mnapozifuata tamanio zenu mbaya, maisha yenu yatazaa matokeo haya maovu: mawazo machafu, utayari kupata starehe zinazotokana na tamaa, kuabudu vinyago, kufuata maroho (kuhimiza matendo yanayotokana na mapepo), chuki na kupigana, wivu na hasira, bidii kila wakati kujitafutia mazuri, malalamishi na kukosoa, hisia kwamba watu wengine wote wana makosa isipokua wale walio katika kundi lako ndogo, husuda, uuaji, ulevi, sherehe za uovu na mambo yote ya aina hiyo"* (Wagalatia 5:19-21)

Ni dhahiri kutoka kwa vifungu hivi viwili ya kwamba, kando na waumini wote kuwa na uwezo wa kutenda dhambi kama hizi, lakini pia inawezekana kupata uhuru kutokana nazo. Ni muhimu sana kwetu sisi kuamini kwamba inawezekana kuwekwa huru kutoka kwa dhambi zinazotufanya kuwa watumwa – bila kujali ni dhabi aina gani.

Pia inastahili kutajwa kuwa kuna sehemu za mtu wetu wa kale ambazo ni mbaya lakini hatuziiti "dhambi". Baadhi ya hizi ni: Wasiwasi, kujihurumia, ukaidi, umaakini uliozidi kuhusu miili yetu, roho ya kulalamika au kukosoa, kupoteza wakati, na kuvunjika moyo. Pia tunaweza kupata uhuru kutoka maeneo haya ya dhambi.

Kwa mfano, tunaweza kuwekwa huru kutoka kwa wasiwasi. Kinachosababisha tuwe na wasiwasi ni kwa sababu tuna mawazo yetu wenyewe ya jinsi maisha yetu ya usoni yanapaswa kuwa. Hivyo basi, wakati mambo yanatendeka na kutufanyaa tufikiri ya kuwa mapendekezo yetu hayatatimia, basi tunashikwa na wasiwasi na kubabaika. Lakini, tukiwekwa huru kutokana na nia ya kufikiri kuwa tunajua kila kitu, tuwekwe huru kutokana na mtizamo wa kibinafsi kuhusu mambo, na huru kutokana na nia ya kujitosheleza wenyewe, basi tutakua huru kutoka kwa wasiwasi na tuweze kuacha mambo yote mikononi mwa Mungu.

Katika Warumi 6:2, Paulo alitufahamisha kuwa waumini hawahitaji kuendelea katika dhambi kwa sababu wao "wamekufa kutoka kwa dhambi". Katika Warumi 6:6, tulijifunza kuwa mtu wetu wa kale amesulubishwa. Na pia kama tulivyokwisha kuona, kuna mambo yaliyo kweli kutuhusu katika maisha ya Kikristo ambayo hatutayapitia mpaka tutakapoamini kwamba ni ya kweli kwetu na



Amri ya nne imepeanwa katika sehemu ya mwisho ya kifungu cha 13, "toa sehemu za mwili ………..". Hatustahili kutumia uweza wetu wa kuongea au kupendekeza maoni yetu, ila inatupasa kuachilia uweza huo kwa Mungu. Kwa maneno mengine, hatuna haki ya kuongelesha wengine kuhusu yale ambayo tunataka kuzungumzia; wala hatuna haki hata ya kukaa kimya. Utawala huo tumemwachia Mungu. Viungo vyote vya mwili wetu tumeviweka chini ya utawala wa Bwana. Paulo anatuambia kwamba wakati Mungu anatumia viungo vya miili yetu, anavifanya kuwa vifaa vya haki. Kwa hivyo, kupitia kwa miili yetu, Mungu atafanya matendo ya haki.

Kumbuka kwamba amri hizi zinategemea utiifu wetu kwa amri zilizotangulia katika mlango wa sita wa Warumi. Uweza wetu wa kutoa viungo vya miili yetu kwa Mungu itawezekana wakati tutakataa kupeana miili yetu iwe chini ya utawala wa dhambi, pamoja na wakati tutakapojipeana kwa Mungu kama wale ambao waliosulubishwa, wakazikwa na kufufuka.

Zisome tena amri tano za kuishi kwa neema.

*Tambua (amini) kwamba umefia dhambi na uhai kwa Mungu.*
*Usiruhusu dhambi kutawala mwilini mwako hata ukaitii.*
*Usiachilie sehemu yoyote ya mwili wako kwa asili yako ya dhambi.*
*Jiachilie kwa Mungu kama mtu ambae amesulubishwa, akazikwa na kufufuka.*
*Achilia viungo vya mwili wako ili Avitumie kufanya matendo ya haki.*

**SURA YA SABA: MAISHA YA KUJAZWA NA ROHO**

Hata kama mtu haisomi Agano Jipya kwa undani, hawezi kuepuka mafundisho yake ya kuwa Yesu anaishi ndani ya waamini wote. Warumi 8:9 inatangaza, *"Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake."* Naye Paulo katika Wagalatia 2:20 anasema, *"Kristo yu hai ndani yangu."*

Kulingana na vifungu vingine katika Biblia, Mungu Baba na Mungu Roho pia huingia au hukaa ndani ya waaminio. Katika Yohana 14:23, Yesu anasema, *"Mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake."* Na katika Yohana 14:16-17, Yesu aliahidi wafuasi Wake kwamba Roho Mtakatifu aliyekuwa *pamoja* nao, atakuwa *ndani* yao. *"Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu."*

Hata kama inatutia moyo kuwa na hakikisho kamili kwamba Kristo yuko "ndani" yetu, tusiwahi kufikiria kwamba uwepo wake pekee ndio tunahitaji. Ni lazima "awe nyumbani" ndani yetu vile vile. Hiyo inamaanisha kuwa ni lazima tuendelee kujazwa kwa Roho Mtakatifu.
Paulo anaandika katika Waefeso 3:14-17, *"Kwa hiyo nampigia Baba magoti, ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa, awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani. Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani."*

Kwa sababu Kristo yuko "ndani" yetu, inawezekana sisi tupate kujazwa kwa Roho Wake. Hata hivyo, ni lazima tuelewe kwamba ni lazima *tujazwe* kwa Roho wa Kristo. Hatuwezi kujijaza wenyewe.

Wengi wetu tumejua kutahayarika wakati tunatafuta ujazo wa kuendelea wa Roho Mtakatifu. Tulikuwa tumepokea ujazo huo wakati tulipompokea Yesu kama Bwana na Mwokozi. Baada ya hapo, tumepata vionjo vidogo vidogo vya ujazo. Lakini, kati ya yote tuliyojaribu, hakuna iliyotuletea ujazo wa kuendelea wa Roho.

Sehemu mojawapo ya kushindwa kwetu ilisababishwa na kutoelewa. Kwa hivyo tunahitaji kuangalia baadhi ya vifungu muhimu katika Maandiko, vitakavyotusaidia kuona vile tutaweza kuingia katika maisha ya kuendelea kujazwa kwa Roho.

Paulo anatuamuru tujazwe kwa Roho katika Waefeso 5:18. Hii inakusudiwa kuwa tendo la kuendelea. Ukweli huu peke yake unastahili kutushawishi kwamba Bwana anatamani tujazwe kwa Roho kila wakati. Wakati tunatambua kwamba ni tamanio Lake kutujaza, tunatambua kwamba mzigo wa kujazwa sio wetu.

Jambo lingine ambalo linatujulisha kwamba tunaweza kujazwa kwa Roho Mtakatifu ni kuwa hatujapatiwa amri ya kujijaza wenyewe. Kinyume na hiyo, tumeambiwa <u>tujazwe</u>. Tunapaswa kuendelea kupokea ujazo wa Roho ambaye amekuwa akitafuta kutujaza na yeye Mwenyewe kuanzia dakika tuliyompokea Yesu kama Mwokozi wetu.



tunapoendelea kujazwa kwa Roho. Bwana wetu ameahidi, *"Yeyote anayeniamini, kama Maandiko yalivyo sema, mito ya maji ya uzima itatiririka kutoka ndani yake"* (Yohana 7:38). Msitari wa 39 unatufunulia kwamba maji yanazungumza kuhusu Roho Mtakatifu. Ahadi sio kwamba "kijito kidogo" cha maji yenye-uzima kitatiririka kutoka kwa wale wanaoishi maisha ya kuendelea kumtegemea. Wala sio "mto" mmoja utakaotiririka. Lakini ahadi ni kwamba "mito" mingi ya maji yenye-uzima itatiririka kutoka kwa wale wanaoendelea kumwamini. Na tumeona kwamba tokeo moja ya kujazwa kwa Roho Mtakatifu ni imani. Mito hiyo itatiririka kwa walio okoka na ambao hawajaokoka. Waliopotea tutawaleta kwa Kristo, na waliokoka tutawaongoza kwa maisha yenye utele. Kuzaa matunda kwa namna hii, kunawakilisha mabadiliko makubwa sana, kwa baadhi yetu ambao tumeng'ang'ana sana kuyagusa maisha ya wengine kwa wema na kwa ajili ya Mungu. Kugundua na kutambua maisha ya kuendelea kujazwa kwa Roho Mtakatifu kunasababisha mabadiliko makubwa ya kushuhudia katika waumini wengi – mabadiliko yanayosababisha ongezeko la uzalishaji wa matunda.

Mabadiliko mengi yaliyotajwa hapa ambayo yanazaliwa katika maisha yetu wakati tunapoendelea kujazwa kwa Roho Mtakatifu, yanatambulika lakini bado hayajafikia utimilifu. Hata hivyo, baadhi yametajwa kwa matumaini kwamba, yatatupatia tamanio la kujazwa kwa Roho. Tunaweza kuendelea kupata ujazo wa Roho Mtakatifu, dakika kwa dakika, kwa kuishi maisha yetu yaliyo unganishwa na Kristo katika kusulubishwa, kuzikwa na kufufuka. Bila kukawia, natuanze sasa kuishi maisha katika umoja wetu na Kristo na kutambua maisha ya kubarikiwa kwa kuendelea kujazwa kwa Roho Mtakatifu.

Warumi 8:1-4 inaweka wazi kwamba, hatudumishi Amri ya Mungu kwa kujaribu kuidumisha, ila ni kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Tunapozisoma Amri Kumi, tunaweza kutambua ikiwa tunazidi kujazwa kwa Roho Mtakatifu – kwa sababu, haki ya sheria inatimizwa kwa wale wanotembea katika Roho. Paulo pia anafundisha katika Warumi 13:8 kwamba, *"Yule anayempenda mwanadamu mwenzake ameitimiza sheria."* Tayari tumeona kwamba tunda la Roho ni upendo. Kwa sababu ya umoja wetu katika Kristo, tunaweza kutembea katika Roho, na hivyo kuweza kuishi katika upendo. Wakati tunaishi katika upendo, ndipo tunapo ambatana na sheria.

Kuwa uhusiano mzuri na watu wengine ni somo la kawaida zaidi katika Bibilia hata kuliko uhusiano wetu na Mungu. Sio la muhimu zaidi, lakini linapatikana zaidi. Na ni mtu yupi ambaye hajateseka kutokana na uhusiano mbaya katika kiwango cha binadamu ? Tunakaribisha msaada wowote unaopatikana katika husiano zetu na watu wengine. Hakuna chochote, ila kujazwa kwa Roho, ndio kutaleta ushindi unaohitajika.

Kitu muhimu zaidi ambacho tunakihitaji tunapokumbana na watu wengine, ni uvumilivu. Tunda la Roho ni uvumilivu. Uvumilivu ni tafsiri ya neno ambalo ni muunganisho wa maneno mawili ya Kiyunani, "hasira" na "mbali zaidi". Yaweke pamoja na unapata "mbali zaidi na hasira". Ndoa, jamii, makanisa na hali zingine ambako unapata husiano zilizovunjika, zingeokolewa kama kungekuwa na utoshelezaji mzuri wa "hasira mbali zaidi". Tutembee katika umoja wetu na Kristo na tupokee ujazo wa Roho Mtakatifu ambao utaleta matokeo ya uvumilivu kwa watu wengine.

Tunda la Roho ni upole. Neno lililo tafsiriwa 'upole' linabeba wazo ya utu wema ndani yake. Tofauti iliyoje inayoletwa na utu wema! Katika ulimwengu unaofafanuliwa kwa tabia zenye ubinafsi kama ujeuri, hasira na chuki, utu wema ndio utakaoweza kujenga husiano zilizovunjika. Utu wema ulio ndani yetu una faida ya ziada ya kuwafanya wengine kujisikia wamefurahiwa – ambayo hiyo siyo huduma ndogo.

*"Nyenyekeeni mmoja kwa mwingine kutokana kwa kicho cha Kristo"* (Waefeso 5:21). Tunaponyenyekea kwa wengine, tunajiweka chini yao. Kunyenyekea ni kinyume cha kujaribu kuwatawala wengine. Uchambuzi wa mjadala wa kifungu chetu unatufunulia ya kwamba, unyenyekevu ni tokeo la kujazwa kwa Roho. Kwa uwazi, roho ya unyenyekevu ndio msingi wa husiano dhabiti katika wanadamu.

Pia tunahitaji "umoja katika Roho" (Waefeso 4:3). Wakati Roho Mtakatifu anapopata njia katika mioyo ya Wakristo, anawaunganisha pamoja katika kifungo dhabiti cha umoja. Kwa hakika, moyo wa Mungu huvunjika anapo ona husiano zilizovunjika kati ya watoto wake. Bila shaka, moyo wake husisimka, Roho Mtakatifu anaporuhusiwa kutufunga pamoja katika roho ya umoja. Zaidi ya kitu kingine chochote, hii roho ya umoja kati ya waumini ndiyo ambayo Bwana wetu aliombea katika ombi Lake kuu lililonakiliwa katika Yohana mlango wa 17. Waza kuhusu mguso tunaoweza kufanya katika ulimwengu ambao haujaokoka watakapotuona tukiwa tumefungwa pamoja kwa Roho anayekaa ndani yetu. Kwa ajili Yake na kwa ajili yao, tutembee katika umoja wetu katika Kristo.

Ujazo wa Roho Mtakatifu unatufanya kuwa Wakristo wanaozaa matunda. Watumishia wote wa Bwana walio waaminifu kikweli, hawatosheki na uzalishaji wao wa matunda. Wanatafuta ongezeko la uzalishaji matunda kwa ajili ya Mungu. Tutakumbana na ongezeko la namna hiyo



Sasa tumefikia swali muhimu: "Ikiwa Roho Mtakatifu anataka kutujaza kwa dhati na sisi pia tunatamani kujazwa kwa dhati, basi mbona haiwi hivyo?" Jibu lake ni rahisi sana. Katika Wagalatia 5:17, Paulo anasema, *"Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamuwezi kufanya mnayotaka."* Hivyo tunaweza kuona kwamba, ikiwa tunatafuta kujazwa kwa Roho lakini hatujazwi, kizuizi kiko mwilini. Lakini, je, kuna jambo linaloweza kutendeka kuhusu kizuizi cha mwili, ili tupate kujazwa kwa Roho? Ndio! Shukuru Mungu, mwili umesulubishwa na kwa hivyo unaweza kuondolewa mamlakani na kung'olewa kama kizuizi cha kujazwa kwa Roho.

Katika Wagalatia 5:24, tunasoma, *"Na hao walio wa KristoYesu wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake."* Hii inamaanisha kwamba ushindi unawezekana! Mara ile tuliyomwamini Kristo, mwili wetu pamoja na shauku zake na tamanio, ulisulubishwa. Wakati mwili unaposulubishwa, haututawali tena, ila Roho Mtakatifu anakuwa huru kutawala maisha yetu.

Keti kwa utulivu sasa mbele za Bwana. Fanya uamuzi wa kuazimia kwamba utaondoa imani yako kwako mwenyewe na ushawishi kwamba u mwenye hekima. Wachana na mipango yako na nia ya kufikiri kwamba unajua kila kitu. Tamani mipango ambayo Mungu amekupangia, kwa ajili ya wengine na ya Ufalme wa Mungu. Sasa amini kwamba mwili wako umesulubishwa. Mwambie Bwana, "Bwana wangu, hivi sasa napokea ujazo wa Roho. Ninajua amekuwa akitafuta kunijaza kuanzia wakati ambapo nilikuwa Wako." SASA UMEJAZWA KWA ROHO MTAKATIFU.

Kumbuka kwamba amri ya Paulo katika Waefeso 5:18 inaonyesha kuwa tunastahili kuendelea kujazwa kwa Roho. Waamini wengine wametambulishwa kama "wajazwa-Roho" kana kwamba wamefikia mahali spesheli katika maisha yao ya kiroho. Lakini hiyo si kweli. Wakati Paulo aliandika hii amri kwamba tunastahili kuendelea kujazwa, alijua kuwa ujazo mmoja hautoshi. Na hakuna kitu kama waumini wafike mahali katika maisha yao ya Kikristo ambapo wanaweza kutambulishwa kama "wajazwa-Roho". Ni lazima tujazwe tena na tena.

Mwili wetu haufi kwa urahisi. Utaendelea kurudi katika utawala. Njia pekee ambayo mwili unaweza kuendelea kukaa bila nguvu ni kwa kuendelea kuukataa na kuamini kwamba umeshasulubishwa. Endelea kujazwa kwa Roho! Fanya hivyo kama ulivyojazwa mda mfupi uliopita.

Hivi sasa tutatazama baadhi ya Baraka nyingi ambazo tunazipokea tunapojazwa kwa Roho.

**SURA YA NANE: TOFAUTI ILETWAYO NA ROHO**

Kuna tofauti kubwa kati ya maisha yetu ya kale ya "kutia bidii kwa kazi ya Yesu" na maisha mapya ya kupokea ujazo wa Roho wa Kristo. Maandiko yafunua huduma nyingi za Roho Mtakatifu. Mlango huu unatuonyesha baadhi ya hizo huduma.

Maisha ya Mkristo ni ya kukua na tusidhani kwamba kuazia wakati huu na kuendelea tutazidi kujazwa kwa Roho Mtakatifu. Kila siku tunaweza kukua katika mwelekeo wa kuendelea kujazwa zaidi. Mabadiliko tunayoweza kuyatarajia ni: Mabadiliko ya kibinafsi, mabadiliko katika uhusiano wetu na Mungu, mabadiliko katika husiano zetu na watu wengine na mabadiliko katika utumishi wetu wa Kikristo.

Haya mabadiliko yote yaliyotajwa hapa, yanapatikana kama matokeo ya kujazwa kwa Roho. Juhudi yeyote ile kutoka kwetu ya kusababisha mambo haya kutendeka hayatafua dafu. Tukijipata bila ya sehemu ya mambo yaliyotajwa hapa, uhitaji wetu ni kupokea ujazo wa Roho Mtakatifu, wala sio kujaribu kuzalisha mambo haya katika maisha yetu. Ijapokua mabadiliko haya ni katika maisha yetu ya kibinafsi, yatajitekeleza katika kila eneo la maisha yetu. Hapa kuna baadhi ya baraka na mabadiliko, tunayoweza kutarajia kama matokeo ya kujazwa kwa Roho.

Tunda la Roho ni furaha. Furaha ni mojawapo ya vitu adimu. Kwa wengi wetu, inategemea juu ya vifungu vya hali zilizo njema. Wakati tumejazwa kwa Roho, tunakua na furaha bila kujali hali zilivyo.
Tunda la Roho ni amani. Hii inamaanisha kua tuna amani ndani yetu. Pia inamaanisha kwamba tuna amani kwa Mungu na kwa watu wengine (wakati wameruhusu). Inasisimua kujua kwamba siku iliyojaa mambo magumu, majonzi, kukata tamaa, hatia, chuki, kupigana na vita, tunaweza kua watoto wa amani katika kujazwa kwa Roho.

Tunda la Roho ni utu wema. Karibia wazazi wote huwafunza watoto wao kua wema. Ila Yesu anasema kua ni Mungu peke yake aliye mwema. Basi ikiwa ni tuwe wema, tutaweza kua hivyo wakati Mungu ni mwema ndani yetu. Naye Mungu ni mwema ndani yetu wakati tu ambao tumejazwa kwa Roho Mtakatifu.

Jambo lingine ambalo Roho Mtakatifu atalizalisha katika maisha yetu ni kujizuia. Neno hili, kujizuia, linatokana na maneno mawili yanayo maanisha, "kuwa na uwezo". Roho Mtakatifu anazalisha uwezo ndani yetu. Hii inamaanisha kua mtu "hajapoteza usukani", ila yuko huru kuitikia matakwa-huru yake mwenyewe ya kuongozwa na Bwana.

Mara nyingi katika Maandiko, Roho Mtakatifu anaitwa Roho wa ukweli. Katika Johana 16:13, Yesu anasema kua Roho Mtakatifu atatuongoza katika kweli yote. Katika Johana 14:26, anasema kua Roho Mtakatifu atatufundisha mambo yote. Paulo anatuambia katika 1 Wakorintho 2:9-10, kua Roho Mtakatifu atatufunulia mambo ambayo Mungu amewaandalia wale wanaompenda. Wakati ambao Roho Mtakatifu anayajaza maisha yetu, sisi tunakua na chanzo kisichopungua cha mwanga wa kiroho. Na huo mwanga unatuagaza kila wakati.

Yesu pia akasema, *"Mshauri, ambaye ni Roho Mtakatifu, atawakumbusha mambo yote ambayo nimewaambia."* (Yohana 14:26). Wengi tumeshangazwa wakati tunatoa ushuhuda na ghafla tunakumbuka kifungu cha Maandiko ambacho hatujakiwaza kwa miaka mingi. Roho Mtakatifu



hutenda kazi kwa njia hiyo katika kila eneo la maisha ya waumini ambao wanaendelea kuishi kuambatana na maisha yaliyojazwa kwa Roho.

Roho Mtakatifu pia anatupatia "uzima katika miili yetu ya muda". Hii inamaanisha kua anatuweka huru kutokana na hisia zinazonyonya nguvu zetu kama vile: uoga, wasiwasi, kufinyiliwa kimawazo, hasira, uchungu, na chuki. Anafanya hivyo kwa kutuweka huru kutokana na kufanya maamuzi. Ni lazima tukumbuke kwamba tunapotembea katika Roho, Bwana anafanya maamuzi kwa niaba yetu nasi tunaitikia maamuzi hayo. Pia, kuna wakati ambao Bwana anatuongoza kufanya mambo ambayo hatuna nguvu za kimwili za kutosha kuyafanya. Kwa wakati kama huo, Roho Mtakatifu atatufungulia raslimali ya nguvu za kimwili na uwezo wa kufanya mambo hayo tuliyoongozwa na Mungu kuyafanya.

Paulo asema tunastahili kuwa: *"Tukiomba kila wakati kwa kila namna ya maombi na kutoa hoja zetu katika Roho"* (Waefeso 6:18). Maombi yetu hubadilika tunapo omba kama tunavyo ongozwa na Roho Mtakatifu. Hatutapoteza wakati mwingi, hoja zisizostahili zitapungua, ufahamu wetu wa mahitaji ya kuombea utaongezeka, na bila shaka hisia zitapungua na tutakuwa na amani zaidi mioyoni mwetu kwamba Mungu atayajibu maombi yetu.

Jambo lingine tutakaloliona ni ongezeko katika shukurani zetu. *"Tukitoa shukurani kila wakati katika mambo yote kwa Mungu Baba"* (Waefeso 5:20). Hii kutoa shukurani hubadilisha maisha ya watoto wa Mungu. Watu wengine wameinuliwa kutoka kwa kufinyiliwa mawazo wakati walipoanza kumshukuru Mungu katika hali zao zote. Shukurani kama hizo hudhihirisha imani yetu kwamba Mungu anatawala hali zetu zote. Kumshukuru Bwana kwa kila jambo sio jambo la kawaida. Ila, wakati tumejazwa kwa Roho, tutaendelea kumshukuru kwa ajili ya mambo yote.

Uhusiano wetu na Mungu ni uhusiano unaokua. Hapa kuna baadhi ya njia ambapo uhusiano huo utazidi kukua kadri tunavyo endelea kujazwa kwa Roho.

Tunda la Roho ni upendo. Bwana wetu anasema amri iliyo kuu zaidi ni tumpende Bwana Mungu wetu kwa mioyo yetu yote, akili, nafsi, na nguvu. Kisha anaongeza kwamba, tunastahili kuwapenda majirani wetu kama tunavyojipenda. Kwa hivyo, mwelekeo wa kwanza wa moyo uliojazwa na Roho Mtakatifu, ni kwa Mungu. Tunapoendelea kupokea ujazo wa Roho Mtakatifu, kunakua na ongezeko la bubujiko la upendo kwa Mungu.

Tunda la Roho ni unyenyekevu. Bwana wetu anasema kwamba wanyenyekevu watairithi inchi. Pia anatuambia tuichukue nira yake juu yetu kwa sababu Yeye ni mnyenyekeve (au mpole). Imesemekana kwa usahihi kwamba "unyenyekevu sio udhaifu." Unyenyekevu ni kuwepo unapohitajika. Bwana hatafuti uwezo wetu, ila uwepo wetu anapotuhitaji. Wakati tunapojazwa kwa Roho Mtakatifu, Mungu anaweza kututumia kama apendavyo.

Tunda la Roho in imani. Mara nyingi, maandiko yanatuhimiza kutamani imani inayokua katika Mungu. Waebrania 11:6 inatuambia, *"Pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu."* Tutakua na imani inayokua tunapoendelea kupokea ujazo wa Roho Mtakatifu.

Warumi 8:14 inasema, *"Wale wanao ongozwa na Roho wa Mungu ndio wana wa Mungu."* Hapa tunaona dhahiri kwamba tunapo jazwa kwa Roho, pia tuta ongozwa na Roho. Na tunapo endelea kuongozwa na Roho, tutatembea katika mapenzi ya Mungu.